BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,010,689,585/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 5

**ZIARA** za Rais Samia ughaibuni zalipa uwekezaji




UKURASA 11


Nipashe
Jumatano Juni 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580991
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Serikali yabariki kusamehe kodi

**Ni** kwa walipaji mahiri, hoja kinzani zaibuliwa.. *ukurasa 2*



Mwigulu Nchemba



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi wa Chama cha ACT - Wazalendo katika utaratibu wake wa kawaida wa kukutana na vyama vya siasa nchini, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Taifa, Juma Duni Haji na Katibu Mkuu Ado Shaibu. **PICHA: IKULU**

# Mbunge ashtukia jambo idadi ya watalii, mapato

UKURASA 2

# Polisi yanasa watuhumiwa wa utapeli mtandaoni

UKURASA 2

**MICHEZO** **PAZIA LIGI KUU KUFUNGWA LEO** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Polisi yanasa watuhumiwa utapeli mtandao

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia Marry Sibora (23) na Zainabu Omary (23), wote wakazi wa Dar es Salaam, kwa tuhuma za kusambaza picha za ngono na kufanya biashara ya ukahaba kwa njia ya mtandao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, jeshi hilo kwa kushirikiana na timu ya kuzuia na kupambana na uhalifu mtandaoni na polisi mkoani Morogoro, pia limemkamata Julius Mwabula (20), mkazi wa Morogoro na wenzake 22, kwa tuhuma za kufanya uhalifu kwa njia ya mtandao.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakijifanya wakuu wa shule, waganga wa kienyeji, ndugu wa waathirika wa matukio mbalimbali, watoa huduma wa kampuni za simu (customer care) au mawakala wa Freemason.

Alifafanua kuwa kupitia mbinu hiyo, watu hao huwatumia watu ujumbe mbalimbali kupitia namba tofauti za simu wakionyesha nia ya kutaka kuwasaidia, kisha huwaibia.

"Watuhumiwa hao wamekutwa wakiwa na vifaa mbalimbali ambavyo wanavitumia kufanya uhalifu huo ikiwamo kompyuta mpakato mbili, kompyuta ya mezani, simu za aina tofauti 28, flash mbili, modem ya mitandao yote na kadi za simu za mitandao mbalimbali zaidi ya 50," alibainisha Kamanda Muliro.

Alisema kuwa moja ya ujumbe unaotumwa kwa watu na wahalifu hao wanapotaka kufanya utapeli ni "Hallo, ndugu mzazi mwanao shuleni amepatwa na matatizo na anaumwa sana, hivyo tuma pesa haraka ili nimpeleke hospitalini" na mhalifu huyo anatoa namba ya kutuma pesa na mtu akituma, anakuwa ameibiwa.

Alitoa onyo kwa watu wanaojihusisha na uhalifu kwa njia yoyote ikiwamo ya mtandao, akisisitiza serikali na vyombo vyake vimejipanga kupambana na uhalifu wa aina yoyote, pia wahalifu watatafutwa popote walipo, kukamatwa na kupelekwa mahakamani.

Alisema watuhumiwa wote waliokamatwa wamehojiwa kwa kina na taratibu za kisheria zinakamilishwa ili wafikishwe mahakamani, huku akitoa wito kwa Watanzania kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa sheria wanapotumia mitandao.

"Jeshi la Polisi linatoa rai kwa Watanzania wote kutumia mitandao kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na kuwa waangalifu na vitendo vya utapeli, ikiwamo kuchukua tahadhari wakati wa kutuma pesa au kufanya biashara katika mitandao ili kuepuka kutapeliwa, pia watu wajiepushe kufanya biashara haramu mitandaoni ikiwamo ya ngono," alisema.

# Serikali yabariki kusamehe kodi

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imebariki hoja yake ya kuwatambua na kuwasamehe walipakodi mahiri, huku mbunge mwenye hoja kinzani akiendeleza msisitizo wake kwamba anaona ishara ya kasoro na kashfa.

Akizungumza bungeni jijini hapa jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali imezingatia dalili zote za walakini kabla ya kuupa baraka msimamo wake huo.

Kwa mujibu wa Dk. Nchemba jana kwenye mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka huu, miongoni mwa yaliyozingatiwa yanajumuisha mapitio ya vyombo vya ulinzi na usalama, kisha kubarikiwa na kikao cha Baraza la Mawaziri.

Akichangia mjadala huo, Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, aliyeasisi mada hiyo katika kikao cha Bunge awali, alitoa angalizo kwamba baraka hiyo ya msamaha inaweza kukaribisha hatari ya Rais kushauriwa vibaya, pia kufungua milango kwa kashfa za rushwa na ufisadi.

Mpina aliyewahi kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alisisitiza kwamba hatua hiyo ya Waziri wa Fedha na Mipango kupewa mamlaka ya kuwatambua walipakodi mahiri na kuwasamehe, ina hatari ya kuua morali kwa wawekezaji wa ndani, watakaonekana siyo mahiri kwa mtazamo wa waziri.

Alitaja maeneo ya hatari hizo, ni pale Rais ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kutoa msamaha huo, anaweza kushauriwa vibaya na baadhi ya watendaji na ikaleta shida kwa nchi.

"Ikiachwa hivyo serikali itakumbwa na kashfa, tutaweka wapi sura zetu na kwa nini tumweke?

"Kwa nini kuwa na misamaha ya kundi na mtu mmoja mmoja na kusema watu mahiri? Hii itaondoa ushindani. Kuna watu watasamehewa na wengine hawatasamehewa na wanaenda kushindana sekta moja," alisema.

Alifafanua ishara iliyo mbele ya hatari hiyo ni kufungwa viwanda huku vingine vikiendelea, msingi wa tatizo ukianzia katika tafsiri za misamaha hiyo ya kodi.

"Mimi napendekeza kama ni miradi ya kimkakati inahitaji msamaha, tuitungie sheria iletwe bungeni kwa utaratibu. Tukiacha hivi, watu watatumia nafasi hii kufanya ufisadi na tutaua uwekezaji nchini," aliwasilisha.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (katikati waliosimama), akishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya usafirishaji wa sampuli za kibaiolojia kati ya Posta Masta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbondo (kulia waliokaa) na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Tutume, Misana Manyama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge ashtukia jambo katika utalii

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

MBUNGE wa kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, ameshangazwa na namna Tanzania Bara ilivyo na vivutio vingi vya utalii, lakini inakusanya mapato kidogo huku Zanzibar yenye idadi ndogo ya vivutio ikipokea watalii wengi.

Nahida amependekeza mambo matatu ya kubadilisha hali hiyo, ikiwamo serikali kuwaagiza mabalozi wote wa Tanzania katika nchi mbalimbali duniani kutoa taarifa ya hatua zitakazochukuliwa kukuza utalii kwa kujifunza huko waliko.

Akichangia mjadala wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 bungeni jijini hapo jana, Nahodha alisema hatua nyingine ni kuweka mfumo wa kukusanya mapato hayo ambao utaonekana Wizara ya Fedha na Mipango na kuimarisha chuo cha utalii kwa kujifunza kwa nchi jirani.

Nahodha alisema idadi ya watalii wanaotembelea nchini na kiwango cha mapato havilingani na uzuri wa nchi, na kwamba nchi jirani zina vivutio vichache lakini idadi ya watalii na mapato yake ni makubwa.

Alitoa mfano kwamba Zanzibar yenye vivutio vya magofu na fukwe inapokea watalii 500,000 ilhali Tanzania Bara yenye hifadhi za Taifa 22, inapokea wageni 800,000 kwa mwaka.

"Tanzania Bara fukwe zipo, magofu ya kale na mbuga za wanyama. Nahisi kuna tatizo au takwimu hazikusanywi kwa usahihi au huduma hazijafikia kiwango cha kuridhisha ama ni ghali," alisema.

KODI YA ARDHI

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi, alikosoa adhabu iliyowekwa mtu akichelewa kulipa kodi ya ardhi kwa miezi sita, riba ni asilimia ya 0.1 na akichelewa zaidi ni asilimia moja.

Pia alisema kuna mazingira ya rushwa yanatengenezwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya asilimia 10 ya mauziano ya nyumba au kiwanja na kwamba wengi hawalipi kodi hiyo na kushauri iwe asilimia tano.

Kunambi aliishauri serikali kuweka maofisa maalum wa kusimamia machinga ili kuwatambua na kujua ukuaji wao na kuchangia kuongeza mapato kuliko hali ilivyo sasa.

## HABARI KITAIFA

# Kibano kikali kwa vigogo halmashauri hoja za CAG

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amekutana na mameya na wenyeviti wa Halmashauri wa Tanzania Bara na kuwapa maagizo mazito ya usimamizi wa matumizi ya fedha za halmashauri.

Fedha hizo ni zinazoelekezwa kwenye matumizi mbalimbali ikiwamo miradi ya maendeleo, ikiwa ni sehemu ya hoja za CAG katika ripoti yake mpya ya mwaka 2020/21 inayofanyiwa kazi na Bunge kwa sasa.

Akifungua mafunzo kwa viongozi hao jana jijini hapo, Majaliwa alisema kuna udanganyifu mkubwa kwenye halmashauri.

"Kama sisi viongozi wa kisiasa kwenye halmashauri tusipokuwa makini tutadanganywa sana na atadanganywa hadi Mkaguzi wa Hesabu, hili limejitokeza Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha atakuwa shahidi na madiwani, limepanga uboreshaji wa barabara zake mjini kuweka kifusi, ni azimio la watu wenye mamlaka likapokelewa na watendaji, utekelezaji wake sasa."

"Fedha ya kwenda huko kwenye barabara ya mtaa inaingizwa kwenye akaunti ya mtu binafsi tukiwa tuna ofisi ya kata na vijiji vina akaunti zake kwanini isipelekwe kwenye akaunti ya mtaa, kijiji au kata? Tunamwekea Mkuu wa idara tena hana mahusiano na barabara kabisa, tulipoibua pale watu walidhani ni mpango tu, lakini kila kitu kimeonekana, tumempeleka CAG mwenyewe," alisema.

"Tunajua nyie sio sehemu ya ubadhirifu, lakini mnaletewa taarifa tumetumia Sh. milioni 200 kwa ajili ya kupeleka vifusi, lakini hizi barabara zipo mitaani kwenu na vifusi vinapakiliwa huko, tunataka muwe makini kwenye maeneo haya hasa mnapofanya kazi na watendaji wetu, lazima mfuatilie halmashauri yako isitumike kama eneo la kuchukulia fedha," alisema.

**SHERIA CSR KUREKEBISHWA**

Hata hivyo, alisema serikali inakusudia kufanyika marekebisho ya Sheria ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) kutokana na kuwa kichaka cha ubadhirifu.

Alisema fedha ya CSR kwenye maeneo yenye miradi ikiwamo Geita huko nyuma walikuwa wanaibiwa sana.

"Tulikuwa tunaambiwa CSR Geita ni Sh. bilioni 10, shule wanazitambua wao, shule inajengwa kwa Sh. bilioni 1.5 wanatumia halmashauri zetu wanafanya kama rubber stamp kupitia matumizi ya Sh. bilioni 1.5 wakati sisi tunajenga shule kwa Sh. milioni 400, tunapitia sheria ili fedha hizi ziletwe kwenye halmashauri zenyewe ndio zijengwe," alisema.

Alisema suala la usimamizi wa mapato atakuwa mkali kwa kuwa ni eneo muhimu kwa serikali na linahitaji uimarishaji ili halmashauri zijiendeshe.

Kuhusu usimamizi wa miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Majaliwa alisema ameanza kuona maeneo kadhaa hayazingatii ubora na mbio za Mwenge zinawapa mrejesho.

"Mbio za Mwenge zinatupa mrejesho kwamba kuna kazi huko hazifanyiki vizuri, pale ambapo kiongozi wa mbio za Mwenge anashika dirisha kukagua na kuondoka nalo kwenye jengo jipya maana yake hakuna ubora," alisema.

Alitaka viongozi hao wafundishwe namna ya kusimamia miradi ili thamani ya fedha ionekane.

"Nendeni mkaimarishe usimamizi wa miradi ya maendeleo hili ni agizo maalum la kusimamia na kuimarisha miradi tunataka tuone ikidumu zaidi na serikali kupitia mapato yake mawili ya ndani na serikali kuu mhakikishe mnapita wenyewe kwa macho yenu na mnakagua."

"Na wala msisite kukemea nyie mmechaguliwa na wananchi na hawa ni watumishi wa umma ndiyo wanaratibu kama wanafanya mambo hayastahili kwenye halmashauri yako kemea, hakuna atakayekutoa kwenye mamlaka yako kemea, viwango vinahitajika na mikataba misimamie na iwe na maslahi kwa wananchi," alisisitiza.

Aliagiza usimamizi wa utawala bora na sheria ili kusaidia kuimarisha mfumo wa usimamizi wa migogoro huku akitaka wananchi wapate taarifa za maendeleo na wasomewe mapato na matumizi ya serikali kuanzia ngazi ya vijiji.

**USIMAMIZI FEDHA**

"Simamieni matumizi ya fedha zilizokusanywa lazima mjue matumizi ya fedha kwenye halmashauri, Mwenyeviti wa halmashauri mjue kwenye halmashauri kila sarafu inayoingia."

"Fedha inayoingia mwenyekiti hajui inafanywa siri watu wanakimbizana wakiulizwa imeingia Sh. milioni 500 ya ujenzi wa shule, hatupeani taarifa, hapana haikubaliki, simamieni fedha, Rais anataka matumizi ya fedha za serikali kwa malengo yaliyokusudiwa."

**MATUMIZI BILA VIELELEZO**

Alisema kuna tabia ya kufanya ununuzi bila vielelezo na kuagiza kuwa ununuzi wa kila siku unapaswa kuwa na nyaraka.

Alikemea matumizi ya fedha bila kupeleka benki huku wengine wakizima mashine za kukusanya mapato (POS) kwa kisingizio cha kutokuwapo kwa mtandao.

**UNUNUZI VIFAA HEWA**

Alisema amebaini ununuzi wa vifaa hewa hasa kipindi hiki cha utekelezaji wa miradi ya muda maalum.

"Nimegundua dosari nyingi hata kwenye miradi ya UVIKO... mradi wa zahanati, kituo cha afya unajengwa kwenye kata, kamati ya ujenzi mwenyekiti ni Mkuu wa Idara, Katibu ni Mkuu wa Idara halafu wananchi wao ni wafuatiliaji tu, ni kutengeneza ubadhirifu wananchi washindwe kuhoji," alisema.

**UREJESHAJI MASURUFU**

Akizungumzia miradi kutekelezwa bila kurejesha masurufu, alisema: "Nimezunguka kwenye miradi yote nimekuta eneo moja tu Nachingwea ambao wametumia na fedha zimebaki wamerejesha, nimeenda kukagua ujenzi wa jengo la upasuaji kulibaki na Sh. milioni 38, kwenye shule zilibaki Sh. milioni 18."

Alisema amekagua maeneo mengine kwenye miradi ya fedha za UVIKO hakuna fedha zilizobaki.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Innocent Bashungwa, alisema mafunzo hayo ya siku mbili yameandaliwa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa viongozi hao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA UTEKELEZAJI**
**(Asilia Shauri la madai Na. 3/2019,)**

**AZANIA BANK LIMITED............................................ MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**BNN ROYAL PALM HOTEL**
**MTWARA LIMITED ........................................... MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

KWA: **BNN ROYAL PALM HOTEL**
**MTWARA LIMITED**
**S.L.P 21077**
**DAR-ES-SALAAM**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 13/7 /2022 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 15/06/2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

**A. H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MTWARA**

DEPUTY REGISTRAR INCHARGE
HIGH COURT OF TANZANIA
MTWARA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **29.06.2022** hadi **30.06.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili:

**KCJ943F/ZE1097, KCM104W/ZF0174**
**KBQ622Z/ZE0978, KCK293W/ZE2585**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
**Urefu - Mita 21 Upana - Mita 4.15 Kimo - Mita 5.15**

3. Njia itakayotumika: **Holili** hadi **Moshi** kupitia **Soweto**, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

216998001



**UBALOZI WA MAREKANI NA DENMARK DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani na Denmark, watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha na Magari **tarehe 2 Julai, 2022 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:Sofa set, Recliner, China base, Hutch, Office desk, Book Shelve, Carpet, Vitanda, Magodoro, Garden table/Chairs, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, Dish washer, A/c split units, Photocopy M/C, Laptop, Medical Delivery Bed, Simtank na vingine vingi.

**Magari, yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land cruiser Prado TX S.Wagon | 1KD Diesel Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 1 | Land Rover Free Lander S. Wagon | SALFA Petrol Engine | 2010 | Haujalipwa |
| 1 | Ford KUGA Station Wagon | GD Petrol Engine | 2016 | Haujalipwa |
| 1 | Honda Motorcycle ACE 125 | 125 CC Petrol Engine | 2011 | Haujalipwa |
| 1 | Mitsubish Shogun Station Wagon | 4M41 Diesel Engine | 2008 | Haujalipwa |
| 1 | Mitsubish Canter Truck / Crane 3 Tons | 4D32 Diesel Engine | 2008 | Umelipwa |
| 1 | Ford Ranger Pick up Singal Cabin | PF2 Diesel Engine | 2014 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 30 Juni mpaka 1 Julai 2022, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 8 Julai, 2022 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.
7. Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka au Sanitaiza.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

216922901

# Mikakati yasukwa serikali kuuza nyama kimataifa

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imesema imeanza kuweka mikakati ya kudhibiti milipuko ya magonjwa katika mifugo, ili kukidhi vigezo vya kuuza nyama kimataifa.

Mojawapo ya mikakati hiyo ni kuanza utambuzi na usajili wa mifugo yote nchini kwa njia ya kielektroniki, kila kijiji kuwa na josho la kuogeshea ng'ombe, na kila mfugo kupatiwa dawa kitaalamu.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alitoa maelezo hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliohusu faida ya safari aliyofanya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini Oman Juni 12, mwaka huu.

Waziri Ndaki alisema hapa nchini kuna viwanda vinne vya kuchakata nyama, lakini vyote vina uwezo mdogo wa kuchakata.

Alisema viwanda hivyo vina uwezo wa kuchakata nyama kwa asilimia 30 hadi 40, hali inayosababisha Tanzania kuwa na uwezo mdogo wa kusafirisha nyama kimataifa.

"Tumejipanga kudhibiti hali ya magonjwa na kukidhi vigezo vya kuuza nyama katika nchi za Saudia na Oman. Kwa sasa tuna uwezo wa kusajili na kutambua mifugo yote kwa njia ya kielektroniki.

"Hadi sasa tumeshawatambua ng'ombe milioni tatu, ikifika Septemba mwaka huu tutakuwa tumekamilisha utambuzi. Tunataka kufahamu kila nyama inatoka wapi, tumejipanga kuhakikisha ng'ombe wetu wanapata dawa, wanaogeshwa sambamba na kila kijiji kuwa na josho la kuogeshea kwa sababu majosho yanazuia magonjwa kwa asilimia 95," alisema Waziri Ndaki.

**USAFIRISHAJI NGOZI**

Waziri Ndaki alisema ngozi zinazozalishwa nchini, asilimia 95 hazina ubora, hali inayosababisha kutokidhi vigezo katika soko la dunia.

Alisema wafugaji wengi wanatumia mbinu ya kupiga chapa mifugo hali inayosababisha kupunguza ubora wa ngozi na kukataliwa kimataifa.

Kadhalika, katika kutatua tatizo hilo, alisema serikali imeanza kutoa elimu kwa wafugaji, kuanza kutumia mbinu ya kisasa ya utambuzi wa mifugo kwa kuwavalisha hereni mifugo.

Alisema pia serikali imeanza kutoa elimu kwa wanaochuna ngozi za wanyama ili wachune kisasa, na utumiaji wa visu vinavyofaa katika uchunaji.

**ZIARA OMAN**

Waziri Ndaki alisema ziara aliyofanya Rais Samia nchini Oman itasaidia kuongeza mauzo ya nyama nchini humo na kuleta fedha za kigeni.

Pia, Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) itanunua mifugo mingi kutoka kwa wafugaji na kuisafirisha kwenda nchini humo.

Faida nyingine aliitaja kuwa ni kampuni za Oman kuja Tanzania kuwekeza, kujenga viwanda vya kuchakata nyama hali itakayoongeza upatikanaji wa ajira.




Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi (watatu kulia), akitoa elimu ya kuijengea jamii uwezo wa kujihoji iitwayo 'Chora Ramani', kwa viongozi wa vikundi na wanajamii, kituoni hapo juzi, ili kushiriki vita dhidi ya vitendo vya ukatili. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vikundi vyadaiwa mil. 204/- mkopo halmashauri

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wameuagiza uongozi kuvisaka na kuvichukulia hatua vikundi vilivyochukua mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 204.3 na kukaidi kurejesha.

Madiwani hao walitoa msimamo huo jana wakati wa kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani kilichokuwa kinajadili hoja za ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2020/21, mjini hapa.

Mmoja wa madiwani hao, Anthony Kayombo, alisema ifike wakati uongozi wa halmashauri kuvifuatilia vikundi hivyo vinavyohusisha vijana, wanawake na wenye ulemavu vilivyonufaika na mikopo hiyo inayotokana na asilimia 10 ya mapato na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Hii changamoto ya madeni ya mikopo imekuwa hoja ya muda mrefu sasa...nashauri hivi vikundi kwa kuwa vipo na vilipewa hii mikopo kwa kufuata utaratibu basi vitafutwe ili vilipe...vikishindwa viongozi wake wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ikiwamo mahakamani," alisisitiza Kayombo.

Hoja hiyo pia uliungwa mkono na Diwani Gabriel Kimamala, aliyetaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuingilia ili kusaidia kunusuru fedha hizo za umma zinazopotelea mikononi mwa watu wachache.

Alisema TAKUKURU inapaswa kuingilia kati ili kuwabana viongozi wa vikundi hivyo ili waweze kurejesha fedha hizo ambazo zinapaswa kukopeshwa vikundi vingine vyenye sifa stahiki.

Akiwasilisha taarifa ya hoja za Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Mweka hazina wa halmashauri hiyo, Piniel Mbura, alisema pamoja manispaa hiyo kupata hati safi, inakabiliwa na tatizo la ukusanyaji wa madeni na kwamba jumla ya Sh. 759,975,000 hazijakusanywa kutoka kwa wadaiwa.

Alisema halmashauri inaendelea na jitihada za kukusanya fedha zote zilizopo nje ikiwa pia ni sehemu ya kujibu hoja hizo za hesabu za serikali kwa mwaka huo wa fedha.

# Mwanafunzi VETA atengeneza roboti kuvitambua vilipuzi

**Na Elizabeth Zaya**

MWANAFUNZI wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi (VETA) Kigoma, Innocent Simon, ametengeneza roboti (military security Robort), kwa ajili ya kusaidia kutambua vilipuzi na mahali vilipotegwa vifaa vya milipuko katika masuala ya ulinzi katika jamii na maeneo ya matukio yenye hatari ya vita au uvunjifu wa amani.

Amesema roboti hiyo inaweza kufanya kazi hiyo kwa kutumia rimoti ya betri au umeme kwa kusimamiwa na mtu ambaye huiendesha bila kuwa eneo la tukio kwa umbali wowote.

Akizungumza na Nipashe kwenye banda la VETA katika Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), Innocent alisema roboti hiyo ina uwezo wa kuvitambua hata kama vimefichwa kwa utalaam mkubwa.

"Kwa mfano kama kuna mahali kumetegwa mabomu au vilipuzi vyovyote, roboti hii ina uwezo wa kutoa taarifa kwa kutoa ishara ya sauti na kuonyesha mahali kilipuzi kilipo kwa sababu kimefungwa kamera," alisema Innocent.

Pia, alisema ikitumika itarahisisha kazi ya doria ambayo hufanywa na jeshi la polisi usiku.

"Kwa mfano ile kazi ya doria ya ulinzi inayofanywa na jeshi la polisi usiku, hii roboti inaweza kusaidia katika hilo, kwa hiyo hata kama askari wanakwenda inakuwa rahisi wanakuwa na muongozo," alisema Innocent.

Kazi nyingine ni kusaidia kutambua mahali vilipofichwa vilipuzi au milipuko na kurahisisha kazi kwa majeshi au walinda usalama kukabiliana na adui kwa urahisi hususani katika maeneo ya vita au mahala panapopangwa kufanyika uhalifu.

Pia, alisema sehemu nyingine roboti hiyo inaweza kufanya kazi ni maeneo ya bandari na viwanja vya ndege.

"Mfano kwenye viwanja vya ndege, inaweza kutumika kusaidia katika suala la ukaguzi kwa ajili ya kubaini wahalifu wanaojaribu kupita na dawa za kulevya au bidhaa yoyote haramu," alisema.

"Kwa sasa hii ambayo nimeitengeneza ni kwa ajili ya maonyesho, lakini ikiboreshwa zaidi na kuwekwa vifaa vya kisasa inaweza kufanya ulinzi kwa ardhini na angani."

HABARI KITAIFA

# Ziara za Rais Samia nje zaleta neema uwekezaji

**Na Gwamaka Alipipi**

ZIARA za Rais Samia Suluhu Hassan alizofanya katika mataifa mbalimbali zimeongeza uwekezaji nchi na kufikia Dola za Marekani bilioni 9.2 (Sh. trilioni 21), mauzo ya nje yakifika Dola bilioni 10 (Sh. trioni 23.2).

Hayo yalibainishwa jana Ikulu jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Profesa Godius Kahyarara, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya ziara ya Rais Samia nchini Oman, Juni 12, mwaka huu.

Profesa Kahyarara alisema takwimu hizo ni kuanzia Juni, mwaka jana hadi Machi mwaka huu.

"Haya yote ni matokeo chanya ya filamu ya The Royal Tour, ziara za Rais Samia nje ya nchi na jitihada nyingine za serikali.

"Kufikia hatua hii ni jambo la kushangilia kwetu kwa sababu kupitia Royal Tour faida kubwa tutakayoipata kwa kuongeza watalii itatusaidia sana kuongeza zaidi mauzo nje."

Alisema mikakati ya serikali hadi ifikapo mwaka 2025 ni mauzo ya bidhaa nje ya nchi kufikia angalau asilimia 30 ya Pato la Taifa (GDP), hali ambayo alieleza inaweza kufikiwa kutokana na kasi ya mauzo ilivyo nje ya nchi.

"Sasa hii maana yake nini, yatatusaidia kutuletea ahueni kwenye deni la taifa. Tukiongeza mauzo nje tunapunguza makali ya deni la Taifa," alisema.

**ROYAL TOUR**

Profesa Kahyrara alisema baada ya kuzinduliwa kwa filamu ya The Royal Tour, watalii na wawekezaji katika sekta ya utalii wameongezeka, kwa mujibu wa hoteli za kitalii Dar es Salaam ongezeko la wageni limefikia asilimia 280 na Arusha asilimia 340.

Alisema kwa upande wa viwanja vya ndege miruko ya ndege imeongezeka ikiwamo ndege zinazoingia nchini.

"Kuanzia Juni mwaka jana na sasa mashirika mengi yameongeza miruko ya ndege hapa nchini, kwa mfano Shirika la Ndege la Oman miruko imeongezeka kutoka miwili hadi saba kwa wiki, Kenya (19-22), Shirika la Ndege la Emirate (4-7), Uturuki (4-7), Fly Dubai (10-4).

Pia ikilinganishwa na kipindi cha nyuma, baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona na baada ya Royal Tour mashirika ya ndege mengi ya kimataifa yameanza kuleta ndege nchini.

"Kwa wastani ongezeko la safari hizo za ndege ni kutoka 93 mpaka 124 kwa wiki."

**UWEKEZAJI**

Vile vile, uwekezaji nchini umeongezeka kwa kiasi kikubwa, akitolea mfano wa mwekezaji mmoja kutoka Marekani ambaye amekuja nchini kujenga hoteli za kisasa za kitalii katika maeneo ya Serengeti, Ngorongoro, Arusha, Zanzibar, Mwanza na Dar es Salaam.

Alisema mwekezaji huyo ameshafika katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) na ameahidi hadi kufikia mwaka 2024 atakuwa amekamilisha ujenzi wa hoteli hizo.

Profesa Kahyarara alisema serikali imejipanga kuhakikisha hoteli zote za kitalii zilizositisha huduma kutokana na matatizo mbalimbali zinaanza kutoa huduma.

## Walia soko sangara kuporomoka bei

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAVUVI wa samaki aina ya sangara wamelia kuporomoka kwa bei ya bidhaa hiyo baada ya wamiliki wa viwanda vya kuchakata minofu kusitisha uzalishaji kutokana na soko walilokuwa wakiuza nje ya nchi kushuka.

Kilio hicho kimetolewa jana jijini hapa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wavuvi Nchini (TAFU), Jephta Machandalo, alipozungumza na Nipashe kuhusu upatikanaji wa samaki katika Ziwa Victoria.

Machandalo alisema kwa sasa wavuvi wengi hawauzi samaki katika viwanda kwa kuwa vimesitisha ununuzi badala yake wanategemea wateja wa kwenye masoko jijini humo.

Alikiri kuwa kutokana na hali hiyo kwa sasa mtaani bei ya samaki imeshuka kutoka Sh. 10,000 kwa kilo moja ya sangara hadi Sh. 7,000.

Kadhalika, wateja wengine wanaowategemea ni wanaonunua samaki hao kuwagandisha kwenye barafu baada ya kuwapaka chumvi maarufu kama (Kayabo) na kuwauza nchini Demokrasia ya Congo (DRC).

Machandalo alisema kushuka kwa bei ya samaki hao, kumesababisha wavuvi kupitia wakati mgumu kutokana na gharama za kuwatoa ziwani hadi kwa mlaji.

"Bei ya samaki imeshuka mtaani na viwandani hawanunui tena samaki aina ya sangara kwa madai kwamba soko la minofu waliyokuwa wakisafirisha nje ya nchi limeshuka," alisema. Kutokana na hali hiyo, soko wanalolitegemea kwa sasa ni mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na nchi za Kenya na Uganda.

Alisema zamani walikuwa wanauza tani 20 hadi 25 za samaki kwa siku katika viwanda mbalimbali, lakini kwa sasa wanauza mara moja moja kwa kiasi kidogo.

Kwa upande mwingine, Machandalo alisema bado kuna tatizo la uvuvi haramu ndani ya Ziwa Victoria na kwamba hali hiyo isipodhibitiwa kuna uwezekano wa sangara kutoweka.

Alisema kwa sasa sangara ndani ya ziwa anavuliwa kwa njia nyavu za dagaa, ndoano, kokoro, nyavu za nchi sita na katika uvuaji huo wanavuliwa wadogo na wakubwa ambao ni majike wanaotegemewa kwa ajili ya kuzaa.

Katika warsha ya kuangalia njia za kukuza sekta ya uvuvi Kanda ya Ziwa, iliyowakutanisha wadau wa uvuvi, baadhi ya wenye viwanda, iliyofanyika wiki iliyopita jijini hapa, walilalamikia kuporomoka kwa soko la minofu nje ya nchi.

Walisema kutokana na hali hiyo, wengi wao wamesitisha kununua samaki kutoka kwa wavuvi kwa kuwa hawana soko la kuuzia minofu watakayochakata.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

CIVIL/CRIMINAL/APPEAL/APPLICATION NO. 426/08 OF 2018

FROM ORIGINAL DECREE/CONVICTION AND SENTENCE/ORDER IN ..........

CASE NO. .......... OF .......... OF THE HIGH COURT OF TANZANIA

AT MWANZA

The Registered Trustees of SOS children's Villages Tanzania ..... APPELLANT/APPLICANT

VERSUS

Igenge Charles and 9 others ..... RESPONDENTS

TAKE NOTICE that an appeal from the Decree/Conviction and Sentence/Order of the Judge of the High Court of Tanzania at MWANZA

has been presented by the said Appellant and that the bearing of the said appeal/Application will take place at MWANZA on the 12TH Day of JULY, 2022 at 9:00 AM O'clock in the forenoon or on any subsequent day which to this Court may seem convenient.

If no appearance is made or on your behalf by yourself, your pleaders or by someone by law authorized to act for you in this appeal/application it will be heard and decided (*exparte*) in your absence.

Give under may hand and the seal of the Court this 16TH day of JUNE, 2022

To: STEPHEN MOSHA ADV
Neptune Law Attorneys
Plot No. 31, 7th FLOOR
Hifadhi House (NSSF House)
Azikiwe Street /Samora
DSM
0746 299999
For the Applicant

Registrar/Deputy Registrar
Court of Appeal of Tanzania

15752/-82/400m'4up

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
INAYOKETI MWANZA

SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 426/08 YA MWAKA 2018

THE REGISTERED TRUSTEES OF SOS CHILDREN'S VILLAGE TANZANIA ..... MUOMBAJI

DHIDI YA

1. IGENGE CHARLES
2. MASUMBUKO ALON
3. CHACHA MALWA
4. MAMA KUNDI
5. JOYCE MSHABAHA
6. PAULINA
7. JOHN NDAKI
8. ANTHON
9. ZEPHANIA MSHABAHA
10. EDWARD KAZARABANHU

..... WAJIBU MAOMBI

KWA:
1. IGENGE CHARLES
2. MASUMBUKO ALON
3. CHACHA MALWA
4. MAMA KUNDI
5. JOYCE MSHABAHA
6. PAULINA
7. JOHN NDAKI
8. ANTHON
9. ZEPHANIA MSHABAHA
10. EDWARD KAZARABANHU

POPOTE MLIPO

Mnajulishwa kwamba shauri la Maombi ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufani Mwanza tarehe 12/07/2022 saa tatu kamili asubuhi (3:00).

Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au mkiwa na mwakilishi wenu anayetambulika kisheria, Maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 17/06/2022

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

E. G. MRANGU
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

216922401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yawe fursa

**WAKATI** maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (DITF) yakianza rasmi jijini Dar es Salaam, washiriki zaidi ya 3,000 kutoka nchini wanatarajiwa kuonyesha bidhaa zao.

Washiriki wengine kutoka nchi za nje 22 wanatarajiwa kuwa miongoni mwa kampuni 180 za nje zitakazoonyesha bidhaa na kuleta hamasa kwa watu watakaokwenda kutembelea mabanda yaliyoandaliwa kwa ajili hiyo.

Maonyesho hayo ambayo kwa jina maarufu hujulikana Sabasaba, huvuta mamia ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam kwenda kutembelea na kujionea bidhaa mbalimbali zinazoonyeshwa.

Fursa hiyo ya kufanyika maonyesho hayo kila mwaka haina budi kutumiwa na wajasiriamali kutangaza bidhaa wanazozitengeneza na vile vile kupata ujuzi kutoka kwa wenzao wa nje wanaokuja kushiriki.

Hata wananchi wanaokwenda kutembelea maonyesho hayo ni fursa kwao kwenda kujifunza kutoka kwa wenzao na kujitengenezea ajira.

Maonyesho hayo hayakuandaliwa kwa ajili ya watu kwenda kutembea na kununua bidhaa pekee, bali ni sehemu pia ya kubadilishana ujuzi kutoka kwa watu wanaotengeneza bidhaa zao mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wa ndani kipindi hiki ni muhimu kwenu wa kutengeneza mtandao na wenzenu wa nje katika kukuza biashara zenu na kutafuta soko la nje.

Hakikisheni mnakuwa na vipeperushi vya kutangaza bidhaa zenu na pia kadi za mawasiliano hata mtakapotafutwa iwe rahisi kupatikana.

Kipindi hiki cha maonyesho ni lazima bidhaa mtakazozionyesha ziwe katika viwango vinavyokubalika kimataifa, kuanzia ubora wake na ufungaji utakaomvutia mteja.

Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi na malighafi zinazoweza kutengenezwa bidhaa na kuleta utofauti na zile zinazotoka nje ya nchi.

Kwa mfano tumebarikiwa kuwa na aina tofauti za viungo vya asili vya chakula ambavyo pia hutumika kama dawa ya kutibu maradhi tofauti.

Nchi yetu ina mashamba yanayozalisha viungo hivyo, hasa kwa upande wa visiwani na kama vikitangazwa vizuri soko lake ni kubwa na watu kutoka mataifa mbalimbali hupenda kutumia viungo vyetu.

Wajasiriamali hasa wanawake wamekuwa na mwamko mkubwa wa kubuni vitu mbalimbali kuanzia bidhaa za chakula mpaka mavazi ambavyo wengine hushindwa hata kuamini kama vimebuniwa na kutengenezwa na Watanzania.

Fursa hii muhimu ya maonyesho haya itumike vizuri kuwatoa Watanzania kutoka hatua waliyopo kwenda mbele zaidi hadi kufikia ya kimataifa.

Tumeelezwa kuwa maonyesho ya Sabasaba yanatambuliwa na Umoja wa Taasisi zinazoandaa ulimwenguni, jambo ambalo linavuta nchi nyingi zilizopata mwamko kushiriki maonyesho hayo.

Uzuri wa maonyesho hayo hushirikisha wafanyabiashara wakubwa na wadogo hali inayotoa fursa ya wadogo kujifunza kwa wenzao na hatimaye wafikie malengo yao ya kuwa wafanyabiashara wakubwa baadaye.

Maonyesho hayo pia ni fursa kwa vijana kupata ajira za muda mfupi zikiwamo za kutangaza bidhaa za kampuni mbalimbali na pia ni sehemu ya kupata njia ya kuwasiliana na wenye kampuni, viwanda, ofisi kupata ajira za muda mrefu.

Itafurahisha kuona maonyesho hayo yanapomalizika wananchi wanaona faida ya kutangaza biashara zao na kutengeneza masoko ya nje.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# RC Dar azuru, abadilishe maisha Uwanja wa Fisi

**DAR ES SALAAM** ni miongoni mwa majiji yenye makazi ya walalahoi likiwamo la Uwanja wa Fisi, sehemu yenye watu wengi wenye maisha duni, wakila vyakula kama ngozi za wanyama na bidhaa zilizoisha muda wa matumizi.

Wakazi wake wanaishi katika umaskini, na wengi wanashindwa kumudu chakula bora na mavazi.

Mazingira hayo yanawalazimisha kutegemea vyakula vya bei nafuu na wakati mwingine huuziwa bidhaa ambazo zimeharibika baada ya kupitisha muda wa matumizi.

Ni kutokana na unafuu wake au kutoelewa athari zake kiafya.

Maduka mbalimbali na wafanyabiashara wanauza bidhaa kulingana na mahitaji na uhalisia wa maisha ya wakazi au wateja wao ili kila mmoja apate anachohitaji.

Kwa mfano, madukani sukari, chumvi, majani ya chai na unga vinapimwa na kufunganywa katika karatasi kwa kipimo tofauti ili kuuzwa kwa bei ambayo mteja anaimudu.

Hata mafuta ya kula nayo yana vipimo vidogo ili kuwapa wateja bidhaa kwa thamani ya fedha zao.

Lakini mbaya zaidi, ni kuwapo kwa biashara ya ngono muda wote wa saa 24, hali ambayo inaongeza hatari zaidi kwa wakazi wa eneo hilo.

Ni kutokana na kuambukizwa maradhi ya ngono ukiwamo UKIMWI, mimba za utotoni kwa watoto, maradhi ya kama homa ya ini yote hayo yakienea kwa njia ya kukutana kwa majimaji za mwili.

Ipo haja ya kuchukua hatua madhubuti za kuokoa jamii ya hapo kwa kuipa elimu na kuihamasisha kubadilika.

Wapo baadhi ya viongozi wa serikali na wanasiasa ambao wamewahi kufika eneo hilo na kutoa ahadi mbalimbali za kuliboresha eneo hilo lakini bado hawajazitekeleza.

Utashi wa kisiasa unahitajika ili kubadili matumizi ya eneo kama njia mojawapo ya kumaliza changamoto hizo na kubadili maisha ya Watanzania hao.

Ingekuwa ni vyema kama kutakuwa na uamuzi wa kweli wa kufanya mabadiliko ya matumizi ya eneo hilo badala ya wanasiasa kupita wakati wa kampeni za uchaguzi na kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki.

Kwa mfano aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Paul Makonda, aliwahi kuahidi kuwa nyumba zote za eneo hilo zitabomolewa na kujengwa viwanda vidogo.

Makonda katika ahadi yake alisema, anasubiri wafanyabiashara wapatikane ili kuanza utaratibu wa kulipa fidia kwa kaya zote za 'Uwanja wa Fisi', ili kuwe na sura mpya.

Hiyo ilikuwa ni Novemba mwaka 2016, lakini hadi sasa eneo hilo limeendelea kubaki kama lilivyo, ndiyo maana kuna haja ya awamu ya sita kulitazama upya na kufanya mambo mapya Uwanja wa Fisi.

Maana yangu ni kwamba, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wa sasa, anaweza kuendeleza mkakati huo ulioachwa na Makonda, ili ahadi hiyo itekelezwe kwa vitendo kama sehemu ya uamuzi wa mkoa.

Ni vyema mkuu wa sasa mkoa akapita eneo hilo kujionea hali ilivyo eneo hilo, ili kama itawezekana afanye kama ambavyo Makonda alikuwa amekusudia, au aangalie njia nyingine ya kunusuru wakazi wa 'Uwanja wa Fisi'.

Kwa jumla kumekuwapo na ahadi mbalimbali za kuboresha eneo hilo, lakini haijajulikana ni nini kinakwamisha utekelezaji wake, hivyo ni vyema utashi wa kisiasa utumike kumaliza changamoto iliopo eneo hilo.

Ninaamini kwamba, ni matamanio ya watu wengi wa eneo hilo kuona likiboreshwa, kwani hata Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Muungano ambao eneo hilo liko ndani yake, Joseph Mkunde, anatamani hivyo.

Kiongozi huyo anasema, anasikitika kuona matamanio hayo bado hayajazaa matunda, na kushauri kila linalowezekanalo kuhakikisha wenye nyumba wa eneo hilo wanalipwa ili kupisha matumizi mengine ya Uwanja wa Fisi.

Ninaungana naye katika hilo, kwani kama kutajengwa viwanda vidogo, itakuwa ni rahisi kuongeza ajira na ikiwezekana, wale wanaofanya biashara ya ngono wapewe kipaumbele ili waachane na kazi hiyo.

Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuzuia ukahaba, lakini pamoja na hayo, njia mojawapo ambayo ingesaidia, ni kubadili matumizi ya eneo hilo ikiwamo kujenga viwanda vidogo kama ambavyo Makonda alikuwa ameahidi.



Diwani wa Kata ya Wazo, Leonard Manyama (kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Flamingo Investment, Ernest Magesa (kushoto) na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mabwepande, Colle Sekondo, baada ya uzinduzi mradi wa maboresho ya zahanati ya Madale, Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam jana, ambapo utafanyika ujenzi vyumba vitatu, uzio, maabara pamoja na maegesho ya magari kwa ufadhili wa Magesa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TMEPiD yasisitiza ushiriki wa vijana kamati za afya

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI inayojihusisha na utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana (TMEPiD), imetoa wito kwa wadau na serikali kupitia vitengo vya afya kutilia mkazo suala la kuwashirikisha vijana katika kamati na mijadala inayozungumzia masuala yanayowahusu ili kuwajengea uelewa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao kilicholenga kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili vijana na kuyapatia ufumbuzi, mwezeshaji kutoka TMEPiD, Nelson Chiziza, alitaja baadhi ya changamoto zilizobainishwa na vijana katika tafiti walizozifanya nchini.

Alisema ushirikishwaji mdogo katika kamati mbalimbali za afya kuanzia ngazi ya mtaa, kata na halmashauri ni moja ya changamoto wanazokutana nazo vijana, akidai kwamba mwongozo uliotolewa na serikali unaelekeza kuwe na wawakilishi vijana wakike na wakiume, lakini kwenye utekelezaji haipo hivyo.

"Hilo walisema wao wenyewe vijana, pia walidai kuwa wanapokwenda kwenye vituo vya afya ili wapate huduma baadhi ya watoa huduma hawana muda wa kutosha wa kuwasikiliza, vijana wana kiu ya kutaka kujua mengi kutoka kwao, lakini wanasema hawapati ushirikiano wa kutosha," alisema na kuongeza;

"Pia, walidai kuwa wawakilishi au watoa huduma walio wengi inawezekana hawajapata mafunzo kikamilifu katika masuala ya utoaji huduma iliyo rafiki na vituo vingi vinavyotoa huduma nzuri vina wahudumu wachache," alisema Chiziza.

Maratibu wa Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Dar es Salaam, Agnes Mgaya, alisema katika utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana bado hawajawafikia kama inavyostahili, akibainisha kuwa bado kuna tatizo la mimba za utotoni.

"Kwa Mkoa wa Dar es Salaam tuna asilimia 20 ya mimba za utotoni pia huduma zetu za afya kuwafikia na kuwaongezea uelewa juu ya taarifa sahihi kuhusiana na afya zao bado iko chini, uelewa huwezi kuupima kwa asilimia, lakini bado tunatambua huduma hizi hazijawafikia vizuri," alisema Agnes.

Aliongeza kuwa hayo yanasababishwa na baadhi ya changamoto walizokuwa nazo ikiwamo ambayo taasisi ya TMEPiD inawasaidia kuhamasisha ushirikishwaji wa vijana katika huduma hizo, huku akibainisha kuwa kuna changamoto ya vijana kushiriki katika masuala ya huduma za uzazi wa mpango.

Mratibu wa Mradi wa uhamasishaji wa vijana kushirikishwa katika kamati za afya ya uzazi kutoka TMEPiD, Aneth Tillya, alieleza mradi huo utasaidia vijana katika masuala ya afya na maendeleo kupata taarifa sahihi pamoja na kuwapatia mafunzo ya utetezi makini.

Alisema wamejikita pia kuhamasisha upatikanaji wa huduma rafiki kwa vijana, akibainisha kuwa katika suala la upangaji wa familia, wengi wanashindwa kwenda kupata huduma hizo kutokana na mazingira ya vituo.

"Kwa Dar es Salaam kuna baadhi ya vituo hakuna sehemu ya kusemea, kupitia mradi huu tunategemea vijana ambao hawakuweza kupata hizo huduma wapate pamoja na afya ambazo ni rafiki, wawe na sehemu ya kusemea matatizo yao na kupata suluhu," alisema Aneth.

# Kafulila aamuru hatua kwa wadaiwa sugu halmashauri

**Na Happy Severine,** MASWA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ametoa amri ya kukusanya madeni yote ya wadaiwa sugu wa halmashauri za mkoa vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alisema zaidi ya Sh. bilioni 1.47 hazijakusanywa toka kwa wadaiwa sugu na kukwamisha shughuli za uendeshaji wa halmashauri hiyo ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alitoa amri hiyo jana kwenye kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani kilichofanyika kwa ajili ya kujadili hoja na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Alisema kuna hoja za wadaiwa sugu za mwaka 2020/21 na watu au taasisi wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.47 na kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi kwenye madeni hayo ikiwamo kuwachukulia hatua.

"Halmashauri mnatakiwa kuwa wakali kwenye pesa na madeni ya serikali ambayo mnayadai, wanapokuwa hawalipi wanapunguza uwekezekano wa halmashauri kufanya kazi kwa uwezo wake," alisema Kafulila.

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inadaiwa Sh. milioni 400 na kuomba kupatiwa orodha ya wanaodaiwa ili TAKUKURU na Jeshi la Polisi waweze kuongeza nguvu ulipaji wa madeni hayo.

Kafulila pia aliiagiza TAKUKURU kuchunguza madeni hayo ili waweze kubaini kinga inayowafanya wadaiwa sugu wasiweze kulipa madeni ya serikali na kwamba ni muhimu kulipa madeni halali.

Katika hatua nyingine, alizitaka halmashauri za mkoa huo zinazodaiwa madeni na wazabuni kulipa madeni hayo ndani ya mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha 2022/23 kufunguliwa.

"Wekeni mpango wa kulipa madeni ya watu na taasisi ndani ya mwezi baada ya mwaka wa fedha kufunguliwa, hakikisheni yanalipwa madeni halali ya wazabuni waliotoa huduma na kudai zaidi ya milioni 900," alisema Kafulila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Simon Berege, alisema katika madai ya wazabuni hadi sasa zaidi ya Sh. milioni 147 zimeshaanza kulipwa.

Alisema katika madeni ya wazabuni ya Sh. milioni 209 wameshalipa Sh. milioni 147 na uhakiki wa madeni utakamilika baada ya wiki mbili ya mwaka wa fedha kufunguliwa.

Vile vile, alisema hadi kufunga mwaka wa fedha 2021/22 watakuwa wamefikisha asilimia 120 ya ukusanyaji wa mapato na lengo la ukusanyaji wa mapato ya serikali na mkoa wa Simiyu limeshavuka.

Akisoma taarifa ya Mkaguzi wa Mdhibiti Mkuu wa Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Simiyu, Gwamaka Mwakisyo, alisema kwa hesabu za mwaka 2020/21, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, imepata hati inayoridhisha.

Pia hadi 2021 ilikuwa na hoja 76 na kati ya hizo 50 zimefanyiwa kazi na kufungwa.


## VODACOM TANZANIA PLC

**Sitholizwe Mdlalose appointed as a Non-Executive Director**
The Company announced on 10 May 2022 that Sitholizwe Mdlalose, the Company's Managing Director will be stepping down on 1 July 2022 following his reassignment to Vodacom Group's South Africa operation as the Managing Director. His contribution as the outgoing MD has been invaluable in focusing the organization on strong pillars of growth and expansion. On the back of that success, the Board is pleased to announce that Sitholizwe Mdlalose will join Vodacom's Board as a Non-Executive Director effective 1 July 2022 taking over from Dejan Kastelic who will resign on 1 July 2022.

The Board takes this opportunity to thank Dejan Kastelic for his contribution to the Board and to congratulate Mr Mdlalose on his appointment and look forward to his service on the Board.

**Vacancy for independent Non-Executive Director**
The Board takes this opportunity to thank Ms Winnie Ouko who resigned on 11 May 2022 for her significant contribution to the Board as an Independent Non-Executive Director since 2017 when the company got listed.

Vodacom is looking for a dynamic and visionary leader to fill this position.

**Qualifications**
- A holder of a bachelor's degree in any marketing, actuarial science, economics, law, ICT, engineering, human resources, or related field. A postgraduate qualification in a business-related field will be an added advantage.
- At least 10 years' experience as a director of a medium to large size company;
- More than 5 years' experience as a board member and of a board committee. Board leadership experience with a listed company would be an added advantage;
- Have a thorough understanding of regulatory compliance, board management, and demonstrable commercial and investment acumen;
- A highly networked individual with the ability to build and maintain relationships beneficial to the organization;
- Not involved in any kind of activity or relationships that could even remotely constitute a material conflict of interest to serve as an independent director.

**Key Responsibilities**
- Appointment of the Managing Director and Finance Director;
- Effective oversight of Vodacom Tanzania's strategic direction;
- Approving major capital projects, acquisitions or divestitures;
- Exercising objective judgment on Vodacom Tanzania's business affairs, independent from the management;
- Ensuring that appropriate governance structures, policies and procedures are in place;
- Ensuring the effectiveness of Vodacom Tanzania's internal controls;
- Reviewing and evaluating Vodacom Tanzania's risks;
- Approving the annual budget and operating plan;
- Approving the consolidated annual and interim financial results as well as all communications to shareholders;
- Approving the senior management structure, responsibilities and succession plans; and Information and technology governance.

If you believe you meet the relevant criteria for this role, please submit your application, copies of your academic and professional certificates, testimonials and your detailed curriculum vitae, clearly quoting the relevant reference number VTPL-NED-06/2022

To apply, kindly log onto our service provider e-recruitment platform via https://apply.workable.com/deloitte-eastafrica Applications deadline is 9th July 2022. All applications MUST be submitted through the e-recruitment portal to be considered.

**About Vodacom Tanzania PLC**
Vodacom Tanzania PLC is the leading mobile communication service provider with the fastest data network in the country. We provide a wide range of services for consumers and enterprise including voice, data, messaging, financial services and enterprise solutions to over 15 million customers. It became the first telecommunication company to be listed on the Dar es Salaam Stock Exchange Plc on 15 August 2017.

Deloitte. vodacom

216923402

# Anusurika kifo mgogoro wa wafugaji na wakulima

**Na Christina Haule,** KILOSA

MKULIMA Sadiki Yohana Misiga, mkazi wa Kijiji cha Mbwade wilayani Kilosa mkoani hapo, amenusurika kufa baada ya kuchomwa kichwani kwa kitu chenye ncha kali na wafugaji baada ya kuzuia mifugo isile mazao yake shambani.

Mkulima huyo ambaye ni Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Mbwande, akisimulia tukio hilo wakati Mkuu wa Wilaya hiyo, Alhaji Majid Mwanga, akiwa kwenye ziara kusikiliza kero za wananchi, alisema mnamo Juni 8, mwaka huu, alipigwa nyumbani kwake na kitu hicho chenye ncha kali baada ya kuzungumza na wafugaji ili watoe mifugo yao shambani kwake walipoiingiza shambani kula mazao yake.

Misiga alisema wafugaji hao walimjibu kuwa kijiji hicho ni chao na wao wanang'ang'ania huenda wanataka kufa, ndipo alipoamua kuondoka kwenda kuwatoka ng'ombe shambani.

Alisema kuwa wakati anaingia shambani, alipigwa na kitu hicho kichwani na kupoteza fahamu kwa zaidi ya nusu saa, akiwahishwa hospitalini alikoshonwa nyuzi sita.

Mkulima mwingine aliyejeruhiwa na wafugaji akitetea mazao yake shambani na mkazi wa kijiji hicho, Amina Simon, alisema kijiji hicho kina mchanganyiko wa wakulima na wafugaji na kwamba hilo limekuwa tatizo kubwa kwa sababu wamekuwa wakipigwa, yeye aking'olewa jino wakati akitetea mazao yake shambani.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Alhaj Majid Mwanga, alisema alilazimika kuagiza viongozi wa kijiji hicho kukamatwa na kuchukuliwa hatua kutokana na kushindwa kutimiza majukumu yao ya kazi kwa kumsaidia mkulima kupata haki yake kwa kutoa taarifa ya tukio hilo mapema ili wahusika wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria, kupata adhabu na kuzuia kuendelea kwa migogoro hiyo.

Aliwataja waliokamatwa na polisi wilayani humo kuwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbwande, Huruma Kadiri, na Ofisa Mtendaji Kijiji hicho, Iddi Ng'okwa, huku akiagiza pia Jeshi la Polisi kuhakikisha linawakamata waliofanya tukio hilo wanaodaiwa walikimbia baada ya tukio hilo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Kilosa, Shabani Mdoe, alisisitiza viongozi kujenga tabia ya kutoa taarifa ili wahalifu wote wachukuliwe hatua pindi wanapofanya uhalifu na kwamba eneo hilo ni la wafugaji na wakulima, hivyo wafugaji hawana nafasi ya kujichukulia sheria mkononi.




Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani wa Vodacom Tanzania Plc, Brigitta Shirima (katikati) na Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Usambazaji wa kampuni hiyo, George Lugata, wakikata utepe kuzindua rasmi banda la Vodacom kwenye maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam jana, ambapo mwaka huu kutakuwa na ofa na huduma mbalimbali ikiwamo punguzo la asilimia 10 kwa wateja wanaolipa kwa huduma ya lipa kwa simu. Kulia ni mtoa huduma wa kampuni hiyo, Sarah Stephen. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Umwonapo mtu huyu toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

JUMANNE Majani 'Msafiri' (54), mwenye tatizo la afya ya akili, anatafutwa na ndugu zake baada ya kutoweka nyumbani kwa dada yake maeneo ya Unga Ltd jijini Arusha.

Akizungumza na Nipashe jana Mikocheni, Dar es Salaam, mdogo wake, Salimu Majani, alisema alichukuliwa na dada yake Fatuma Majani 'Mama Khalifa' ambaye ni mke wa Mzee Ngoma ili kupata matibabu.

"Alichukuliwa mwanzoni mwa mwezi huu kutoka nyumbani Ikungi Singida, lakini Juni 13 alfajiri alitoweka na hadi sasa hatujui alipo na tumeshatoa taarifa kituo cha polisi jijini Arusha na kufungua jalada," alisema Majani.

Alisema kuwa alifunguliwa jalada namba AR/RB/6902/2022 13/6/2022, akiwaomba wasamaria wema watakaomwona, watoe taarifa kituo chochote cha polisi au kumpigia simu kupitia namba 0754-991450 au 0762-464630.



# Kampuni ya madini yasaidia madawati

**Na John Badi**

KAMPUNI ya Sotta Mining Ltd (SMCL) inayojenga mradi wa dhahabu wa Nyanzaga, imetoa madawati 190 kuunga mkono jamii inayouzunguka eneo la mradi wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Mbali na madawati hayo, SMCL pia imetoa msaada wa lita 200 za Methylated Spirit kwa ajili ya kutoa matibabu katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na kliniki wilayani humo.

Akipokea msaada huo juzi, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Allan Augustine, aliishukuru kampuni hiyo na kusema msaada huo umethibitisha kuwa ni washirika wakubwa na wa mfano katika maendeleo ya wananchi.

"Tunafurahi kuwa mahali hapa siku ya leo kupokea msaada huu kutoka kwa kampuni hii kuzingatia mpango wa uwajibikaji kwa jamii umeonyesha ushirikiano wa karibu uliojengeka kati yake na Wilaya ya Sengerema," alisema Augustine.

Meneja Mkuu na Mkurugenzi wa SMCL, Damiene Valente, alisema kuwa msaada huo wa tatu kutolewa na kampuni yao kwa jamii hiyo chini ya mpango wa uwajibikaji wa kampuni hiyo na imefurahishwa na ushiriki wa viongozi wa wilaya hiyo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na maofisa kutoka wilaya hiyo pamoja na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa SMCL, wakiwamo wakurugenzi waliotuliwa na Serikali ya Tanzania ambao ni Prof. Raphael Chibunda na Dk. Joas Kabete. Wakurugenzi wengine waliohudhuria ni pamoja na Leonard Mususa.

SMCL ni kampuni inayoundwa na ushirikiano kati ya serikali ya Tanzania (asilimia 16) na Kampuni ya Madini ya Nyanzaga (asilimia 84) ambayo ni tawi la kampuni ya OreCorp Tanzania Limited ili kujenga mgodi wa dhahabu kusini mwa Ngoma wilayani Sengerema wenye thamani ya Sh. bilioni 670 za Kitanzania kufuatia upatikanaji wa leseni ya uchimbaji tarehe 13 Desemba 2021.

Mradi huu uko mbioni kuwa mgodi mkubwa zaidi wa kwanza wa dhahabu kuwahi kujengwa nchini kwa zaidi ya muongo mmoja na wa kwanza kuwahi kujengwa wilayani Sengerema.

SMCL imekuwa ikitoa misaada kwa shule zinazozunguka eneo la mradi, hivi karibuni ikijenga madarasa matatu mapya kwa ajili ya Shule ya Sekondari Ngoma. Pia wamejenga vyoo vipya kwa ajili ya shule hiyo.

Mnamo mwezi Aprili mwaka huu, SMCL ilikabidhi vyoo vipya sita kwa ajili ya Shule ya Msingi Kisiwa cha Chikomero wilayani Sengerema.

Kampuni hiyo pia imekuwa ikiunga mkono mfumo wa afya wa wilaya hiyo kupitia kampeni ya elimu na chanjo dhidi ya UVIKO-19.

Mradi wa dhahabu wa Nyanzaga upo Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kwenye ukanda wa dhahabu wa Ziwa Victoria. Mradi wa Nyanzaga unakadiriwa kuwa na wakia milioni tatu za dhahabu na utazalisha kiasi cha wakia 200,000 (tani sita) za dhahabu kwa mwaka na ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 670.

Mradi huo unatarajiwa kuzalisha nafasi za ajira muhimu na kuchangia uchumi kupitia ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, mirabaha na kodi.

# Mwendokasi yaanza kusafirisha abiria maonyesho Sabasaba

Na Joseph Mwendapole

WAKATI mabasi ya mwendokasi yakianza kutoa huduma kwenda viwanya vya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, jumla ya nchi 22 zimethibitisha kushiriki maonyesho hayo ya 46 yaliyoanza jana.

Ruti ya Gerezani Kariakoo kuelekea Sabasaba ilizinduliwa jana jijini hapo na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade), Latifa Mohamed alisema jumla ya kampuni 3,200 za Watanzania zimethibitisha kushiriki kwenye maonyesho hayo wakati ya kigeni yako 181.

Aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya kufika kwenye maonyesho hayo kutokana na kurahisishwa kwa usafiri watakaotumia wastani wa dakika 10 mpaka 15 kufika kwenye viwanja hivyo kutokea Mbagala na Gerezani.

"Kama zamani walikuwa wanachelewa sasa hivi wamerahisishiwa sana usafiri upo wa kutosha wa kwenda na kurudi muda wa kusubiri mabasi ni mfupi sana na ulinzi na usalama umeimarishwa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama," alisema.

Alisema Tantrade iliamua kushirikiana na DART ili kuwarahisishia wananchi usafiri waweze kufika kwa haraka na kurejea nyumbani mapema tofauti na zamani walikuwa wakitumia muda mwingi.

"Upande wa Mbagala kutakuwa na kituo kikubwa kule Mbagala Rangi Tatu Mivinjeni mabasi yatawaleta hapa na Gerezani Kariakoo watakaletwa hapa kwa nauli ya Sh. 650 tu hivyo tunaomba wajitokeze kushiriki kwenye maonyesho haya," alisema Latifa.

Alisema ushirikiano huo na DART utakuwa endelevu katika kukuza biashara na aliwahakikishia wananchi barabara za mwendokasi kuelekea Mbagala zitakamilika na kuanza kutumika rasmi mwezi Machi mwakani.

Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, alisema maonyesho ya 46 yameanza rasmi na aliwashauri wananchi kujitokeza kushuhudia huduma mbalimbali zinazotolewa.

"Kwa maonyesho ya mwaka huu nawahakikishia mtu yeyote atakayefika hatajutia kuja kwake kwasababu kama mlivyoambiwa kampuni zaidi ya 3,200 ya ndani na kampuni 181 kutoka nje ya nchi yameleta mambo mengi mazuri," alisema.

Kuhusu mabasi ya mwendokasi, Rugwa alisema wameweka kituo kikubwa maeneo ya Gerezani Kariakoo kwasababu ni eneo ambalo linapokea idadi kubwa ya watu kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema wamefanya majaribio ya muda wa kutoka Gerezani kwa kutumia basi la mwendokasi ambapo wametumia wastani wa dakika 12, hali ambayo alisema ni tofauti iwapo mtu angetumia usafiri mwingine.

"Nawahakikishia Watanzania kwa kutumia usafiri huu unaweza kuja Sabasaba ukafanya shughuli zako zote na ndani ya saa moja tu ukawa umemaliza shughuli zako na kurudi mapema sana nyumbani tofauti na ilivyokuwa zamani," alisema.

DART na Tantrade waliamua kurahisisha usafiri ili kuwavutia wananchi wengi kuhudhuria maonyesho hayo bila woga wa kupoteza muda mwingi barabarani hali ambayo ingewafanya waache shughuli zao zingine za kiuchumi.




Meneja Mkuu wa Kampuni ya Specialized Rentals Ltd (SRL), Mihir Patwardhan (kushoto), akikabidhi mfano wa ufunguo wa gari kwa Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael (katikati), kama ishara ya kumkabidhi magari mapya 45 aina ya Isuzu D-Max Pickup, katika ofisi za Kipawa Al Mansour, jijini Dar es Salaam jana, yaliyokodiwa na Kampuni ya Tigo Tanzania, kwa ajili ya kuwahudumia wateja wake nchini kote. Kulia ni Meneja Mkuu wa Al Mansour Tanzania, Anurup Chatterjee. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wadau mazingira wapongeza kupandishwa bei 'baby diapers'

Na Jenifer Gilla

WADAU wa mazingira nchini wameipongeza serikali kwa kuongeza ushuru wa taulo za watoto (Baby Diapers) kutoka asilimia 25 hadi 35 kwa madai kuwa itasaidia kulinda na kuhifadhi mazingira.

Akisoma makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023 bungeni jijini Dodoma mapema mwezi huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inakusudia kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye taulo za watoto zinazotumbulika kwa HS code 9619.00.90.

Alisema lengo la hatua hiyo ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hii nchini, kuongeza ajira pamoja na mapato ya serikali.

Mhandisi wa Mazingira, Dk. Jakobo Kihila, alisema kupanda kwa bei ya bidhaa hizo kutapunguza matumizi kwa baadhi ya watu ambao hawana uwezo wa kumudu gharama zake na kupunguza utupwaji ovyo wa bidhaa hiyo.

"Kwa mfano kwa sasa pampasi inauzwa Sh. 500 dukani sasa baada ya gharama za kodi kupanda inaweza kufika 700 au 1000, kwa hiyo mtu kama alizoea kutumia mbili kwa siku anaweza kulazimika kutumia moja kulingana na kipato chake," alisema.

Mtaalamu huyo wa mazingira alisema kuwa kwa upande mwingine inaweza isiwe suluhisho kwa sababu matumizi hayo yanatokana na mabadiliko ya mazingira na tabia.

Alisema suluhisho la kudumu litapatikana jamii itakapoona umuhimu wa kutunza mazingira na kutumia bidhaa ambazo hazina madhara.

Nyendo Kinyonga mtafiti wa kata jijini Dar es Salaam alisema, ingawa lengo la serikali lilikuwa ni kulinda viwanda vya ndani, uamuzi huo pia una manufaa katika utunzaji wa mazingira kwa bidhaa hiyo ni taka zinazozagaa mitaani na kuharibu taswira ya nchi.

Alisema kupanda kuendane na njia mbadala ya kuhakikisha wale wenye uwezo wa kuzinunua hawaendelezi utamaduni wa kuchafua mazingira.

Vile vile, inahitajika elimu kwa jamii kuhusu madhara yanayoweza kutokea kutokana na kuzagaa kwa taka hizo mitaani na haja ya kutunza mazingira hasa kwa wazazi wenye watoto wanaotumia bidhaa hiyo.

Saraha Pima, Mkurugenzi wa Asasi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), alisema ingawa lengo la serikali kuongeza kodi hiyo ili kuongeza ajira, mapato ya serikali na kuhamasisha ukuaji wa viwanda vya ndani ongezeko hilo litasababisha kupunguza uchafu wa mazingira kwa sababu zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ndizo zinazouzwa bei nafuu.

"Nikiwa kama mdau wa mazingira ninayetembelea maeneo mbalimbali hasa kwenye fukwe za bahari ninashuhudia taka hizi hasa taulo za watoto zikiongezeka siku hadi siku na kuathiri ikolojia ya bahari kwa maana hiyo hizi za nje zinazouzwa bei rahisi zikizuiliwa inamaana watu watakuwa na nidhamu katika kuzinunua za ndani," alisema.

Alitoa rai kwa wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo kuzingatia na kuhusika katika utunzaji wa mazingira kwa kuwa utafiti unaonyesha kuwa diapers zinatumia miaka 500 hadi 800 kuoza na nyingi zinakimbilia baharini na kwenda kuathiri viumbe bahari.

"Wanatakiwa waje na njia bunifu ambazo zitasaidia utengenezaji wa bidhaa hizi ziwe zinaharibika na kupotea katika mazingira ya kwa kuwa kwa jinsi zilivyo zinakaa muda mrefu kwenye ardhi na kusababisha madhara kwa bayoanuai," alisema.

Huku Mwenyekiti wa Asasi ya Kiraia ya Maendeleo Endelevu inayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira (SDN), Freddy Kwezy, alisema licha ya ongezeko hilo kusaidia kulinda mazingira, pia litaokoa watoto dhidi ya magonjwa kama UTI kutokana na wazazi kuwaacha na taulo hizo kwa muda mrefu.

Alisema ongezeko hilo litachochea wazazi kurudi katika matumizi ya nepi kutokana na unafuu wa gharama zake hali itakayosaidia kutunza mazingira na kuwaepusha watoto na magonjwa na ngozi.

## Ufumbuzi changamoto zinazokabili wenye ulemavu waanza utekelezaji

Na Peter Mkwavila, DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Patrobas Katambi, amebainisha utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wenye ulemavu ikiwamo ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi.

Katambi alisema hayo alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Kitaifa wa wafanyakazi wenye Ulemavu ulioandaliwa na Taasisi ya Ikupa Trust Fund uliofanyika Dodoma.

Alisema Rais Samia ametoa zaidi ya Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kukarabati vyuo vya ufundi stadi kwa wenye ulemavu utakaofanyika katika vyuo vinne.

Vyuo hivyo ni pamoja na cha mkoa wa Tabora, Singida, Dar es Salaam na Mtwara, na vitakavyojengwa vipya mkoani Kigoma na Mwanza na Chuo cha Masiwani Tanga kikiwa tayari kimeshafunguliwa.

Alibainisha kuwa tayari serikali imeiwezesha Hospitali ya KCMC kuzalisha mafuta yanayosaidia kukinga mionzi ya jua kwa wenye ualbino ikiwa na lengo la uhamasishaji wa uzalishaji mafuta kwa ajili ya kuleta unafuu na uhakika wa upatikanaji wake.

Katambi alisema katika kuhakikisha haki inatendeka kwa wenye ulemavu, tayari serikali imetoa fedha kwa ajili ya kupitia sera na sheria zinazowahusu wenye ulemavu.

"Sera na sheria hizo ikwamo waraka wa utekelezaji wa sheria ya watu wenye ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010," alisisitiza.

Aidha, sera nyingine ni ya huduma kwa wenye ulemavu ya mwaka 2004 pamoja na kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na sera ya taifa ya vijana zinaendelea kufanyiwa mapitio.

Katika hatua nyingine Katambi alisisitiza ujenzi wa majengo ya serikali unazingatia miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu, na kuzitaka mamlaka za serikali na zisizo za serikali kutekeleza sera na sheria za wenye ulemavu nchini.

"Sera na sheria yetu inasema asilimia tatu katika utoaji wa ajira kwa wenye ulemavu, tunaenda kufanya ukaguzi kwa kuanza na mamlaka za serikali kuona ni namna gani zinatekeleza pia tutaenda kukagua sekta binafsi, tunazitaka mamlaka, asasi na taasisi zisizo za serikali kutekeleza sheria za wenye ulemavu kama inavyotakiwa," alisema.

# Mbunge aomba madaktari bingwa mkoani Mtwara

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameitaka serikali kupeleka madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini, mkoani Mtwara kutokana na kuwapo na daktari mmoja.

Akiuliza maswali bungeni jana, Chikota alisema matarajio ya hospitali hiyo ni kutoa huduma za kibingwa, lakini kwa sasa kuna daktari bingwa mmoja pekee.

"Lini serikali italeta madaktari bingwa ili huduma za kibingwa zitolewe kwenye hospitali hiyo," alihoji.

Aidha, mbunge huyo alisema ili wataalamu hao wafanye kazi kwa ufanisi wanahitaji vifaa na kuhoji lini vifaa hivyo vitapatikana katika hospitali hiyo ambavyo vinanunuliwa kupitia Taasisi ya Ocean Road.

Katika swali la msingi, alihoji lini serikali itapeleka watumishi wa kutosha kwenye hospitali hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alijibu ifikapo Julai, mwaka huu madaktari bingwa watapelekwa na kwenye kibali cha ajira cha sasa madaktari wanane wamepangiwa kwenda kwenye hospitali hiyo.

Kuhusu vifaa tiba, alisema vipo kwenye manunuzi na vinatarajiwa kuingia nchini na ikifika Oktoba, mwaka huu vitakuwa vimefungwa na kuanza kufanya kazi. Awali, alisema hospitali hiyo ilizinduliwa mwezi Oktoba, 2021 ikiwa na watumishi 45.

Alisema kwenye kibali cha sasa cha ajira imepangiwa watumishi wapya 112 itakayofanya idadi ya watumishi kufikia 157, Julai 2022.



Mbunge wa Viti Maalum, Oliver Semuguruka, akiuliza swali bungeni, jijini Dodoma jana, kuhusu lini serikali itajenga kingo za Mto Kanoni unaopita katikati ya Mji wa Bukoba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Hatua nne kuzuia upotevu mapato zatajwa

BUNGE limeelezwa hatua nne za kiukaguzi wa miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya kampuni za kimataifa kwa lengo la kuzuia upotevu wa mapato.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alitaja hatua hizo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni kwa kiwango gani serikali imejiimarisha kukagua miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya kampuni ya kimataifa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema, serikali kupitia Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhusu suala hilo.

Alitaja hatua hizo ni pamoja na kuendelea kuboresha mifumo ya ndani ya ukusanyaji kodi kama vile mfumo wa usimamizi wa mashine za utoaji wa risiti za kielektroniki na mfumo wa kuwasilisha ritani kielektroniki.

Pia alisema kutoa mafunzo ya vitendo kwa watumishi katika nchi mbalimbali zenye uzoefu wa kushughulikia miamala ya uhamishaji wa bei ya mauzo ya bidhaa na huduma baina ya kampuni za kimataifa.

Alibainisha kuwa kuimarisha utekelezaji wa mkataba wa kubadilishana taarifa kati ya Serikali ya Tanzania na nchi zingine na kuendelea kufanya majadiliano na wadau mbalimbali ili kuona uwezekano wa kujiunga na Global Forum on Tax Transparency na ubadilishanaji wa taarifa kwa lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa.

Katika swali lake la nyongeza, alihoji maboresho hayo ni makubwa yamesaidiaje kuongeza kaguzi ikilinganishwa na zilizopita.

"Je, maboresho hayo yaliyofanywa na TRA yamesaidia kuokoa fedha kiasi gani zilizokuwa zikipotea kutokana na kukosekana kwa uwezo ndani ya nchi wa kukagua miamala hiyo?" Alihoji.

Chande akijibu maswali hayo, alisema maboresho hayo yameongeza asilimia 4.5 na kwa mwaka uliopita kabla ya maboresho ilikuwa asilimia 1.2.

## Serikali yafafanua tozo za chakula Bara, Visiwani

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema bidhaa za chakula na mboga halisi zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar hazitozwi kodi, tozo na ushuru wa aina yoyote kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, katika bidhaa za chakula kutoka viwandani hutozwa tozo ya uchakataji nyaraka za forodha ya asilimia 0.6 pekee kwenye thamani ya mzigo huo.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chaani (CCM), Usenge Hamad Juma.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi, tozo na ushuru wa bidhaa za chakula na mboga kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar ili kudhibiti mfumuko wa bei wa bidhaa hizo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande alisema lengo la tozo hiyo ni kugharamia huduma ya uchakataji wa nyaraka za forodha na hutozwa kwa wateja wote wanaotumia Mfumo wa Forodha (TANCIS).

Pia, alisema bidhaa za chakula na mboga halisi hazitozwi tozo ya uchakataji nyaraka kwa sababu hazihitaji kufanyiwa mchakato wa nyaraka katika mfumo wa forodha.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji bidhaa za mifugo hasa ng'ombe na mbuzi kwa Zanzibar ni adimu na bei ya ghali.

"Serikali ina mpango gani wa kufuta au kupunguza kodi zote zinazotozwa bandarini kwa upande wa Tanga na Kisumbwi ili kumpunguzia gharama mwananchi wa Zanzibar," alihoji.

Alihoji serikali lini itatembelea bandarini na kuangalia wananchi wanavyolazimishwa kulipa kodi.

Akijibu maswali hayo, alisema suala la kufuta kodi na tozo amelichukua watalifanyia kazi kwa kuwa ni suala la kisheria huku akiahidi kutembelea bandari kuona hali halisi.




**Habari zote: Augusta Njoji DODOMA**

Ruto shujaa akipambana na dola badala ya upinzani

Ukurasa 13



Ukurasa 14



**WAZIRI MKUU NARENDRA MODI TOKA MATOPENI, KWENYE DUNGU HADI IKULU ILIKUWA DHIKI KUU, AFURAHIA MAMA KUFIKIA MIAKA 100**



# CCM na safari katiba mpya

## •LHRC ina mapendekezo kukwamua mchakato
## •CHADEMA nayo yajiandaa kuutolea tamko

**Na Sabato Kasika**

HATUA ya CCM kutangazia umma kuwa, imekubali mchakato wa katiba mpya uangaliwe kwa maslahi ya taifa, imezidi kuteka hisia za wadau mbalimbali wa siasa, ambao wameendelea kueleza ya moyoni kuhusu azma hiyo. Miongoni mwao ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambacho kinapongeza hatua hiyo, na kupendekeza namna bora ya kufufua mchakato wa katiba mpya.

Lengo ni kuzuia kujirudia yale yaliyotokea katika Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 na kusababisha baadhi ya wanasiasa kususia bunge hilo, LHRC ikidai kuwa chanzo kilikuwa ni ukosefu wa utashi wa kisiasa.

Kituo hicho kinaanza kwa kupongeza maamuzi yaliyofanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya kuridhia kufufua mchakato huo, kulingana na taarifa iliyotolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka.

Mkurugenzi Mtendaji, Anna Henga, katika mhojiano anasema ni ishara nzuri ya kuimarisha demokrasia na haki za binadamu, ambapo anampongeza Mwenyekiti wa CCM Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua hiyo.

### MAKOSA YASIJIRUDIE

Mkurugenzi Mtendaji Henga anasema, ili mchakato ufanikiwe, ni vyema makosa ya awali yasijirudie, kwa maelezo kuwa Bunge Maalum la Katiba la awali lilikuwa na changamoto nyingi, ambazo si vyema zikajitokeza tena.

Katika ufafanuzi wake anasema, baadhi ya wajumbe wa bunge hilo walisusa kupitisha katiba pendekezwa na kusababisha mgawanyiko katika jamii na kuathiri mwenendo mzima wa mchakato wa katiba hiyo.

"Kulikuwa na mabishano ya muundo wa serikali, hoja ya kuwa na serikali moja au mbili, ambapo jambo hilo lilisababisha hoja nyingine ambazo zina umhimu katika jamii kutojadiliwa," anasema Henga.




Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, akizungumzia uamuzi wa CCM kuridhia mchakato wa Katiba Mpya, kulia na Mkuu wa Uchechemuzi wa kituo hicho, William Maduhu na Mkurugenzi wa Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji, Felista Mauya. **PICHA: SABATO KASIKA**.

Ili kwenda vizuri, anasema LHRC ina mapendekezo yatakayosaidia kuendelea na mchakato wa katiba mpya, mojawapo ikiwa ni kufanya mabadiliko ya sheria yote ya Mabadiliko ya Katiba Na. 8/211 na kuweka muundo mpya wa Bunge Maalum la Katiba, ili kuanza majadiliano ya kutunga nyingine.

"Serikali pia ipeleke muswada bungeni wa Mabadiliko ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ili kuunda upya Bunge Maalum la Katiba likiwa na uwakilishi wa wajumbe, tofauti na wabunge wachache wa vyama," anasema. Anasema kituo hicho kinashauri serikali ipeleke bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Kura ya Maoni, ili kuipa uhalali wa kisheria, huku pendekezo jingine likiwa ni Bunge Maalum la Katiba litakaloundwa, litumie Rasimu ya Katiba ya Warioba katika majadiliano.

"Lakini pia tunaishauri serikali kuendelea kufungua milango ya majadiliano miongoni mwa Watanzania kwa njia ya mikutano, makongamano, mitandao, midahalo na vyombo vya habari kuhusu mambo ya msingi na muhimu ndani ya katiba, kwa mustakabali wa taifa," anashauri.

Mapendekezo hayo anayatoa kwa wanahabari, jijini Dar es Salaam alipokuwa akielezea namna bora ya kufufua mchakato wa katiba mpya.

### BADO KUNA UTATA

Mwanasiasa Abdul Kambaya, anasema, bado kuna utata iwapo itafuatwa Sheria ya Uanzishwaji wa Mabadiliko ya Katiba inayomtaka Rais kuteua watu watakaoungana na wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuunda Bunge la Katiba, au inakuwaje.

Anasema, kwa sheria hiyo, vyama vitapaswa kuchukua mjumbe mmoja kutoka bara na mwingine visiwani, na kwamba, kwa hali hiyo, kwa sheria iliyotumiwa kuanzisha mchakato mpya wa katiba analiona litakuwa tatizo.

"Lakini pia swali langu ni hili, kuna viongozi wenye uzoefu na umahiri katika siasa mfano CHADEMA tukiangalia kwa mujibu wa sheria ya muundo wa Bunge la Katiba ni nani kati ya Mbowe, Lissu, Mnyika, Msigwa, Heche, Lema na Salum Mwalimu Naibu Katibu Mkuu Zanzibar ataingia katika bunge hilo iwapo itatumika sheria ya awali? Anahoji Kambaya.

Mwanasiasa huyo pia anahoji kuwa ni nani kati ya wanachama wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, Ado Shaibu, Bashange, Jussa, Mazurui na Juma Haji Duni ambao wataingia katika bunge hilo?

Anaamini wanahitajika wataalamu hao kutengeneza katiba na siyo mtu mmoja mmoja kwa kigezo cha Zanzibar na Tanzania Bara.

"CCM imefanya kikao cha Kamati Kuu na kuridhia kuendelea na kukwamua mchakato wa upatikanaji wa katiba mpya, lakini muhimu ieleweke ni jinsi gani wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba watapatikana," anasema.

Kambaya anasema, haina maana kuendelea na mfumo wa zamani ambao anadai kuwa uliingiza bungeni baadhi ya watu ambao walikuwa na ajenda za vyama vyao badala ya kubeba ajenda za nchi.

### VIKAO VYA TAMKO

Naibu Katibu Mkuu CHADEMA (Zanzibar), Salum Mwalimu, anasema licha ya kwamba chama hicho kinakubaliana na CCM kwenye eneo hilo la upatikanaji wa katiba mpya, watakaa kikao kutoa tamko.

Anasema, suala hilo lina umuhimu na maslahi kwa taifa na kwamba imekuwa ni ajenda kuu na tena ya muda mrefu ya chama hicho kikuu cha upinzani ambayo kimekuwa kikiipigania.

"Sidhani kwamba, kuna mtu asiyejua jinsi ambavyo CHADEMA imekuwa ikipigania hilo, hivyo tutakaa vikao na kutoa tamko kuhusu msimamo huo mpya wa CCM kuhusu Katiba mpya," anasema Mwalimu.

### UAMUZI MPYA CCM

Hivi karibuni, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, aliutangazia umma kuwa chama hicho kimekubali mchakato wa katiba mpya uangaliwe kwa maslahi ya taifa.

Kwamba, katika kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu walichokaa Juni 22 mwaka huu, walikubaliana suala hilo na kwamba chama hicho kinasisitiza umuhimu wa uwapo wa katiba hiyo kwa kuzingatia mazingira ya sasa na kuona namna bora ya kufufua, kukwamua na kukamilisha mchakato wake kwa maslahi ya taifa na maendeleo kwa ujumla.

CCM imekubali kuuhuisha mchakato huo, kutokana na maslahi kwa taifa, hatua ambayo inaonyesha kuwa sasa imeachana na msimamo wa awali wa muda mrefu wa kuhusu kuwapo katiba mpya.

Uamuzi huo mzito kwa siasa za Tanzania, kutokana na upande wa upinzani hasa CHADEMA kudai kwamba haikuitarajia na hivyo kujipanga kukutana katika vikao kwa ajili ya kuutolea tamko.

Mazingira ya siasa yaliyokuwapo miaka sita iliyopita, chama hicho kilikuwa na msimamo tofauti, kufuatia kuweka kando mchakato wa katiba mpya uliokwama mwaka 2014, baada ya kumalizika kwa Bunge Maalum la Katiba.

# Zilivyo njia tofauti kuuelewa mchakato wa katiba mpya




Mwenyekiti wa CCM Rais Samia Suluhu Hassan na chama tawala, wamebariki kuwapo mchakato wa katiba mpya. **PICHA MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

UONGOZI wa CCM 'umekubali yaishe' kumaliza msuguano wa muda mrefu kati ya serikali na vyama vya siasa na makundi ya kiharakati pamoja na wadau kuhusu mchakato wa kuwapo kwa katiba mpya.

Katika mkutano wake na wadau wa siasa kupitia Jukwaa la Demokrasia, Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu, Hassan, alikubali kuwa yaletwe mapendekezo, yaseme ni nini hasa kinatakiwa kubadilishwa katika katiba na kwa sababu gani.

Kila kipengele kitakacholetwa mezani kubadilishwa kijadiliwe kwa kina na kura zipigwe pale itakapobidi.

Mwelekeo huo ulieleweka katika hadhara ambayo iliandaliwa kufanikisha au kuongezea kubadilishana mawazo katika kile kinachotambuliwa kama maridhiano, dhana ya kisiasa ambayo kimsingi ni ya siasa za Zanzibar, iliyoanza kutokana na tofauti za CUF na CCM,

Sababu ni kuwa licha ya hali halisi kwamba upinzani Bara hauna mizizi kama ulivyo Zanzibar, kutokana na kuwepo kwa umoja wa kina zaidi wakati wa kufikia uhuru, upinzani umeendelea kukua kwa kasi na kuwa 'ndani ya 18' za kupata ushindi endapo uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Kutokana na udhahiri wa kukua kwa upinzani na akiwemo mtawala asiyetaka kusikia habari za kugawana madaraka au kutafuta maridhiano endapo upinzani ungefikia karibu nusu ya viti bungeni, matokeo ya uchaguzi mkuu uliopita, ulibakiza wagombea wa CCM pekee.

Kubakiza wagombea wa CCM kwenye ushindani huku wengine wakidaiwa kukosea majina yao wenyewe hivyo fomu zao kutupwa, hali iliyoleta taharuki au mkwamo katika mfumo wa siasa, hivyo maridhiano ni kukubali kurekebisha hali hiyo ili kuendana na mahitaji ya demokrasia, hata kama hali hiyo inaweza kugharimu kiasi fulani kugawana majimbo ya uchaguzi.

Ndiyo hapo linakuja suala la kuridhia mchakato wa katiba mpya kulikotangazwa na chama tawala majuzi tofauti na wengine walivyotarajia kuhusu suala hilo.

Cha kujiuliza hapa ni kama CCM ni ile ile lakini inabadilisha lugha au mbinu za kutetea msimamo wake, na kama ni kweli chama tawala kimebadilika, ni kwa kiasi gani, kwani kimeshapata mwongozo wa mwelekeo wa kujadili hitaji la katiba mpya kutoka kwa mwenyekiti wake.

Kwa maneno mengine, mchakato wa katiba mpya ambao CCM imeuridhia ni ule ambao Rais Samia Suluhu Hassan ameelezea, wa kuleta pendekezo la kubadilisha kipengele fulani katika katiba iliyopo na kukijadili kwa kina kuhusu pendekezo kustahili kukubaliwa au hapana, na ikibidi wajumbe wapige kura.

> Kisiasa, au kwa lugha nyingine 'kwa ujanja wa kisiasa,' kilichokubaliwa katika vikao vya juu vya chama tawala ni kuondoa faida ya kisiasa ambayo upinzani unapata kwa dhana ya katiba mpya...

Kwa maana hiyo shangwe na vifijo vilivyofuatia tangazo kuwa chama tawala kimeridhia mchakato wa katiba mpya inawezekana hazijapata picha halisi ya suala hilo, au sura ambayo ni rahisi zaidi kuwa sahihi kuhusu mwelekeo wa CCM katika suala hilo.

Kinachoweza kuleta shangwe ni hisia kuwa sasa chama tawala kimeelewa na kinakubali haja ya katiba mpya kwa maana ile ya kawaida, hali inayoashiria kuwa siyo ajabu ufanyike mkutano kwa mfano katika Jukwaa la Demokrasia na haja ya kupelekwa bungeni kuanza mchakato wa kupitisha Rasimu ya Warioba au Katiba Pendekezwa.

Kisiasa, au kwa lugha nyingine 'kwa ujanja wa kisiasa,' kilichokubaliwa katika vikao vya juu vya chama tawala ni kuondoa faida ya kisiasa ambayo upinzani unapata kwa dhana ya katiba mpya, uamuzi ambao ni mwendelezo wa ule wa utawala wa awamu ya nne.

Baada ya uchaguzi mkuu Oktoba 2010 na kuapishwa Baraza la Mawazirii mwisho wa mwezi Novemba, wiki mbili za kwanza za mwezi Desemba zilitawaliwa ma miito ya katiba mpya, hasa kutoka kwa viongozi wa makundi ya jamii .

Mwelekeo huo ukatoa uhalali wa kutaka katiba mpya ambayo msingi hasa wa dai hilo ni kutaka Tume Huru ya Uchaguzi, kuruhusu mgombea huru, matokeo ya urais kupingwa mahakamani, kuwapo serikali tatu, kupunguza madaraka ya rais kuteua watendaji na viongozi.

Kumekuwa na mjadala miongoni mwa wanaharakati na wapinzani kama kudai tume huru kuendane na katiba mpya au dai hilo lishughulikiwe kivyake ili limalizwe kabla ya uchaguzi mkuu ujao.

Hapo ndipo sasa itafutwe katiba mpya,ni wazi mwelekeo wa pili una mantiki ila hauna msingi wa kisiasa, kwa maana kuwa tume huru haiwezi kuridhiwa na serikali au chama tawala kwa kutumia katiba iliyopo si jambo ambalo linalazimisha kuhitajika kuanzishwa kwa mchakato wa jumla wa katiba mpya.

Bila kufanya upelelezi wowote, inafikirika bila tatizo kuwa serikali ambayo haina dhamira ya kunyang'anya kura au kung'oa wagombea kwa mabavu inaweza pia kuridhia kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi kama chombo cha kitaifa kinachojitegemea.

Kinaweza kuwa na wajumbe wanaoaminiwa na taasisi tofauti, kwa mfano Mahakama ya Rufani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Shule Kuu ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chama cha Wanasheria Tanganyika na wajumbe wengine watakaoridhiwa kwa msingi wa sheria husika.

Hatua hiyo inaweza kuwa msingi wa katiba mpya, na 'mengineyo' yaletwe mezani baadaye.

WIKI 6 KUELEKEA TAREHE YA UCHAGUZI

# Ruto shujaa akipambana na dola badala ya upinzani

## •Ni king'ang'anizi, haogopi wala kusikia la mtu

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kuungana na William Ruto na kushinda uchaguzi wa 2013 na mara ya pili 2017, Rais Uhuru Kenyatta, kuanzia hapo alisimama na kudhamiria kuwa naibu wake huyo hasongi mbele na kukikalia kiti cha urais kwenye uchaguzi wa 2022.


Kuvunjika kwa muungano wa wawili hao uliondwa kwa jina la Jubilee Party, kulileta usaliti ambao ulimfanya Ruto kuwa jasiri zaidi akisimama mwenyewe na kutaka kuingia ikulu hata kwa goli la kisigino.

Baada ya vijana hao wawili maarufu 'UhuRuto' kushinda uchaguzi mpya wa urais uliokumbwa na utata 2017, ndugu hao wawili wa kisiasa walitazamwa na wengi kuwa wangemaliza muhula wao wa pili kama walivyoanza wa kwanza wakiwa mapacha au timu ya kutisha ya manahodha wenye nia moja, na nahodha kiongozi Uhuru akitarajiwa kumwachia kijiti mwezake mara baada ya muda wake kuisha.

Hata hivyo, hayo hayakutokea na kinachoonekana leo ni mtifuano nahodha hajamwachia kijiti na amesema hafai kuongoza nchi hiyo badala yake Raila Odinga ndiye mrithi wake.

Kama ni bahari imechafuka maji yametibuka marafiki wa zamani hawaogelei tena katika mwelekeo wa pamoja licha ya kwamba wako ndani ya bwawa moja , lakini kuvunjika kwa muungano kuna dalili zote za usaliti,udanganyifu, ulaghai na ujanja.

Chama cha Jubilee huenda hakikutaka kuona mgawanyiko ulivyokuwa unakuja; kama walifanya hivyo, wote walijikausha wasijulikane kama walikuwa na taarifa za tukio hilo.



Wapinzani wakuu kwenye uchaguzi wa mwaka huu Raila Odinga (kushoto ) na Makamu wa Rais William Ruto.

Uongozi wa Serikali ya Kenya na chama tawala ni uwanja wa kambi mbili zinazopingana kikamilifu zinazoongozwa na wahusika wakuu, Rais Kenyatta, ambaye anauunga mkono upinzani chini ya Raila Odinga na Ruto ambaye sasa ni mpinzani akipambana na serikali iliyo madarakani ambayo yuko ndani yake kama Naibu Rais lakini asiyekubalika.

Ruto anafahamu kuwa vita vya sasa vinavyoendeshwa dhidi yake vinapiganwa na watu ambao alidhani ni marafiki zake wa kisiasa na wadau aliowaamini.

Hao si maadui bali anachofanya ni kukabiliana na marafiki wake wa kisiasa ambao wamemgeuzia kibao ambao hapo awali walijifanya watani wake lakini walikuwa wakimfanyia kweli.

Uhuru anatumaini na anaamini kuwa amefanikiwa kummaliza kisiasa naibu wake jambo ambalo pengine Wakenya hawakutarajia, kwa vile Ruto ni rafiki wa miaka mingi.

Licha ya kwamba Ruto sasa ndiye mpinzani kwa hali inavyokwenda ana nguvu na anapambana, hata kama mikakati ya Odinga ilianza kupangiwa ikulu anakofanyakazi Makamu wa Rais, lakini pia yote hayo ni matokeo ya kumsaka mrithi wa uchaguzi wa 2022 na hakuna cha kuficha kwamba Ruto anakihitaji sana kijiti cha kuiongoza Kenya.

### DHANA YA URAIS

Uchaguzi wa Kenya na figisu za Ruto na Kenyatta zinatoa taswira kwamba viongozi au makamu wa marais wa Afrika siyo kwa kificho ni kwa uwazi wakiona rais anamaliza mihula yake wanakitamani sana kiti cha ikulu.

Wanaamini kuwa ikiwa umekuwa naibu rais kwa miaka 10 au saba, unataka nini? Unachotaka kama mwanasiasa ni nafasi ya urais? Ni jinamizi lililopo Afrika na kwenye siasa kwingineko duniani hata Marekani, kwa hiyo Ruto hajakosea alikuwa na kila sababu ya kuwa Rais wa Kenya 2022.

Joseph Biden Rais wa leo wa Marekani alikuwa makamu wa Rais wa Barack Obama, licha ya kwamba hakutaka kugombea urais baada ya Obama kumaliza muhula wake, lakini ni wazi aliutamani.

Aliingia baadaye baada ya miaka minne ya utawala wa Donald Trump, aliyeingia ikulu kwa kumwangusha mgombea wa Obama Hillary Clinton.

Ni kweli pia kwamba mara tu Uhuru na Ruto walipoapishwa kwa muhula wa pili na wa mwisho, wapenzi wa Ruto walianza kumtangaza mgombea wao na lilikuwa jambo la kawaida kufanywa ili kuweka msingi.

### ANA UMAARUFU

Ruto anaibuka kutoka uchaguzi mkuu wa 2007 kama mwanasiasa mashuhuri zaidi wa jamii ya Kalenjin, na kufanikiwa kuhamasisha kiwango cha kuvutia cha uungwaji mkono wa kura dhidi ya katiba mpya mwaka wa 2010.

Michakato mbalimbali ya kisheria ilizua maswali kuhusiana na uadilifu wake na kufaa kwake katika nyadhifa za kisiasa. Jambo la kufurahisha zaidi lilikuwa tangazo la Desemba 2010 kwamba alikuwa akichunguzwa kufuatia uthibitisho wa mashtaka dhidi yake Januari 2012 na Mahakama ya Makosa ya Kibindamu (ICC) iliyoko Hegue Uholanzi akituhumiwa na jukumu lake la madai kuhusika na uhalifu dhidi ya binadamu.

Alidaiwa kuwa ni mshiriki wa uhalifu dhidi ya ubinadamu akidaiwa kuhamasisha mauaji, uhamisho wa watu kwa nguvu kushiriki kwenye mateso katika sehemu za kaunti za Uasin Gishu na Nandi.

Hili ni muhimu kwa kuwa jukumu la uchochezi wa kisiasa katika kuchochea ghasia kati ya makabila tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990 linatambuliwa sana kimataifa ikiwa ni pamoja na Wakalenjin katika Bonde la Ufa, ambao wengi wao wameteseka moja kwa moja au kwa njia nyingine kwa sababu za matokeo ya vurumai za kisiasa zinamhusisha Ruto.

Hata hivyo, Makamu wa Rais anaonekana kuwa ni shujaa anayepambana licha ya kwamba ikulu ilitaka kumweka pembeni, anasema atapambana mpaka kieleweke wiki chache kuanzia sasa.



Enzi za ubia wa kisiasa wa mapacha Rais Uhuru Kenyatta (kushoto) na Naibu Rais Ruto. Wawili hao sasa ni mahasimu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### WAZIRI MKUU NARENDRA MODI

# TOKA MATOPENI, KWENYE DUNGU HADI IKULU ILIKUWA DHIKI KUU, AFURAHIA MAMA KUFIKIA MIAKA 100



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi akizungumza na mama yake, Smt Heeraba alipotimiza miaka 100. **PICHA UBALOZI WA INDIA**

**Na Romana Mallya**

"HUKO mjini Vadnagar, familia yetu ilikuwa ikikaa katika nyumba ndogo ambayo haikuwa na dirisha, vitu muhimu kama choo au bafu, tulikuwa tukiita chumba cha kupanga chenye kuta za matope na vigae vya udongo kwenye paa. Sote kwa pamoja, wazazi , ndugu zangu na mimi tuliishi humo,"

Ni baadhi ya maneno aliyoandika, Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, katika andiko la kuadhimisha miaka 100 ya mama yake, Smt Heeraba.

Ni andiko la mama katika sherehe ya kuzaliwa huku akisema hajawahi kupata ujasiri wa kuandika kwa urefu hadharani kuhusu maisha ya mama yake, taarifa inayotolewa na Ubalozi wa India jijini Dar es Salaam.

"Kila la kheri unapoanza mwaka wako wa kuzaliwa wa 100. ..mama yangu ni wa kawaida lakini wa kipekee, kama ilivyo kwa akina mama wote,"anaeleza.

Anakiri kuwa, mama siyo tu neno kama maneno mengine katika kamusi, hujumuisha hisia mbalimbali kama upendo, uvumilivu, uaminifu, na mengineyo.

Anasema kote duniani watoto wana mapenzi ya dhati kwa mama zao, siyo tu huzaa watoto pia huunda akili , utu na kujiamini kwao.

"Na wakati wa kufanya hivyo, kina mama hujitolea bila ubinafsi mahitaji na matarajio yao binafsi leo Juni 18, 2022, najisikia furaha sana na bahati ya kuwashirikisha kwamba mama yangu, Smt Heeraba, anatimiza mwaka wa 100," anasema.

Anasimulia kuwa hiyo, itakuwa karne moja tangu kuzaliwa kwake, kama baba yake angekuwa hai, angeweza kusherehekea siku yake ya kuzaliwa ya 100 wiki iliyopita.

"Mwaka 2022 ni wa kipekee kwa kuwa mama yangu anatimiza karne moja kipindi ambacho baba yangu angekuwa tayari ameshatimiza karne yake..."

**WAPI ALIKOZALIWA**

Anasema, "Mama yangu alizaliwa katika miji ya Visnagar na Mehsana eneo la Gujarat, karibu na mji wangu Vadnaga. Hakupata mapenzi ya mama yake bibi yangu kwa ugonjwa hatari wa homa kali ya mafua ya Kihispania-Spanish influenza".

"Aliishi katika utoto bila mama, hakuweza kumtukana mama yake kama ambavyo sisi sote tufanyavyo sasa. Hakuweza kulalia paja la mama yake kama sisi sote tulivyofanya, hakwenda shule kujifunza kusoma na kuandika.

"Utoto wake ulikuwa moja ya umaskini na kunyimwa haki zake ikilinganishwa na leo. Utoto wa mama yangu ulikuwa mgumu sana. Huenda hiki ndicho alichokusudia Mwenyezi Mungu kwa ajili yake. Mama pia anaamini kwamba haya yalikuwa mapenzi ya Mungu. Lakini kumpoteza mama mapema katika umri mdogo ni hali iliyoendelea kumpa maumivu." Anasema.

Anasimulia kuwa mama yake hakuwa na utoto mwingi kwa sababu ya mapambano hayo yalimlazimisha akue zaidi ya umri wake, alikuwa mtoto mkubwa katika familia yake na akawa mkwe mkubwa baada ya ndoa.

**FAMILIA ILIKOTOKA**

Waziri Mkuu anasimulia kuwa, mjini Vadnagar, familia yao ilikaa katika nyumba ndogo ambayo haikuwa na dirisha, choo au bafu, na kwamba wote kwa pamoja, wazazi wangu, ndugu zangu waliishi humo.

> "Kuta zilikuwa nyeusi na zenye masizi na zilizohitaji kusafishwa, alifanya kazi hiyo mwenyewe kila wakati na kuifanya nyumba kuwa yetu yenye uchafu kuwa na harufu nzuri, pia alitengeneza bakuli ndogo za udongo ili kuipamba na alikuwa bingwa katika stadi maarufu ya kuchakata vitu vya zamani vya nyumbani."

"Baba yangu alitengeneza nyumba ya mianzi juu ya miti na mbao ili iwe rahisi kwa mama kupika chakula. Jengo hili lilikuwa jikoni. Mama alikuwa akipanda juu ya 'machaan' kupika na familia nzima iliweza kukaa juu na kula pamoja," anakumbuka maisha walikoanzia.

Hata hivyo, anasema wazazi wake hawakuruhusu hofu iliyotokana na mapambano ya maisha ya kila siku kutawala mazingira ya familia, waligawana majukumu yao kwa uangalifu na kuyatimiza.

"Akitumia saa ya ukutani baba alikuwa akiondoka kwenda kazini saa 10:00 alfajiri, aliwapa ishara majirani kuwa ni saa 10:00 alfajiri na kaka yake Damodar aliondoka pia. Ibada nyingine ya kila siku ilikuwa ni kusali kwenye hekalu la karibu kabla ya kufungua duka lake dogo la chai."

"Mama alizingatia muda aliamka pamoja na baba yangu na kumaliza kazi nyingi asubuhi na kwenda kusaga nafaka na kukoboa mchele. Hakuwa na msaidizi wakati akifanya kazi, alikuwa akiwaimbia kwa kukoroma tenzi, nyimbo anazozipenda sana," anasimulia.

**ALICHOPENDA UTOTONI**

Waziri Mkuu Modi anasema alifurahia kuogelea kwenye bwawa la kienyeji na alichukua nguo zote chafu na kuzifua bwawani huku mama yake akiosha vyombo kwenye baadhi ya nyumba ili kusaidia kukidhi gharama za matumizi ya nyumbani pamoja na kuchambua pamba hadi kupata nyuzi.

Hata, katika kazi hii ya kuumiza mgongo, wasiwasi wake mkubwa ulikuwa ni kuzuia miba ya pamba asiwatoboe.Mama hakutegemea wengine wala kuomba msaada. Msimu wa upepo ungeweza kuleta matatizo kwenye nyumba yetu ya matope. Hata hivyo, tulikabiliana na dhoruba ya upepo.

"Katika majira ya joto mwezi Juni, alipanda juu ya paa la matope na kukarabati vigae. Hata hivyo, licha ya juhudi zake za kishujaa, nyumba ilikuwa ya zamani sana kuhimili athari za mvua, wakati wa mvua, paa letu lingeweza kuvuja na nyumba ingedhurika kwa mafuriko, lakini aliweka ndoo na vyombo chini kwenye sehemu iliyokua ikivuja kukusanya maji .

"Hata katika hali hii mbaya, mama alionyesha ujasiri, utashangazwa kwa namna ambavyo alitumia maji hayo kwa siku zijazo, hakika ni mfano mzuri wa uhifadhi wa maji, alikuwa anapenda kupamba nyumba na alitumia muda mwingi kuisafisha na kupamba, akiipaka samadi ya ng'ombe," anasimulia.

Waziri Mkuu huyo anasema samadi ya ng'ombe hutoa moshi mwingi inapochomwa hivyo, mama yake alitumia kupikakatika nyumba isiyo na dirisha.

"Kuta zilikuwa nyeusi na zenye masizi na zilizohitaji kusafishwa, alifanya kazi hiyo mwenyewe kila wakati na kuifanya nyumba kuwa yetu yenye uchafu kuwa na harufu nzuri, pia alitengeneza bakuli ndogo za udongo ili kuipamba na alikuwa bingwa katika stadi maarufu ya kuchakata vitu vya zamani vya nyumbani."

Modi anasema tabia nyingine ya mama yake ni kupenda kwa dhati viumbe hai wengine ambao wakati wa joto aliweka vyombo vya maji ili ndege wanywe, alihakikisha mbwa waliopotea kwa jirani wanakula.

Sifa nyingine anaitaja kuwa alitengeneza samli tamu yenye krimu ambayo baba yake alikuwa akileta kutoka duka lake la chai na hakupenda chakula kitupwe hata punje.

**UWAZIRI MKUU**

Modi anasimulia kuwa baada ya miaka mingi kupita mama yake kila anapoulizwa ni kwa namna gani anajivunia mtoto wake kuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, anajibu ;

"Ninajivunia kama ambavyo wewe unavyojivunia hakuna kilicho changu, lakini mimi ni chombo tu katika mipango ya Mungu kumleta mtoto huyu duniani."

Kiongozi huyo anasema mama yake mara nyingi haambatani naye kwenye shughuli zozote za kiserikali au za umma alifanya hivyo mara mbili hapo zamani.

"Mara moja, ilikuwa katika kazi ya umma huko Ahmedabad wakati alipoiweka alama ya Kihindu "tilak" kwenye paji la uso wangu baada ya kurudi kutoka Srinagar ambako nilipandisha bendera ya taifa huko Lal Chowk".

"Tukio la pili ni pale nilipokula kiapo kama Waziri Mkuu wa Gujarat mwaka 2001, hafla ya kuapishwa ilifanyika miongo miwili iliyopita na ilikuwa hafla ya mwisho ya kiserikali ambayo mama alihudhuria. Anasema waliwahi kumwomba mama yake ahudhurie hafla ya kuwapa heshima walimu wake mbele ya umma, lakini alikataa na kusema, mimi ni mtu wa kawaida tu, labda kwa kuwa nimekuzaa, lakini umefunzwa na kulelewa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu."

Modi amekuwa Waziri Mkuu wa India kwa miaka 14 tangu mwaka 2014 hadi sasa pia alikuwa Waziri Mkuu wa Gujarat kutoka mwaka 2001 hadi 2014 na ni mbunge wa Bunge la Taifa wa jimbo la Varanasi.

Mwaka 2016, Modi alizuru Tanzania pia kuitembelea Afrika kwa lengo la kukuza uhusiano. dishu.





# ‘Wazazi ongeeni na watoto wenu kuchagua marafiki bora’

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na kuongezeka kwa vitendo vya ulawiti kwa watoto shuleni, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wazazi kuzungumza na watoto wao ili kubaini wanapofanyiwa vitendo hivyo.

Shekimweri, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wazazi wa shule za msingi za kata ya Ipagala kwenye hafla ya kuwapongeza walimu kwa kuwezesha idadi kubwa ya wanafunzi kufaulu katika mtihani wa darasa la saba, mwaka jana.

Alisema, wazazi wanapaswa kuzungumza na watoto wao ili wachague marafiki wenye tabia bora kutokana na mmomonyoko wa maadili uliopo hivi sasa katika jamii.

“Wazazi ongeeni na watoto wenu kuchagua marafiki wenye tabia bora kumeibuka tabia za ulawiti kwa watoto mashuleni ongeeni na watoto wenu ili kudhibiti tabia hizo ambazo watoto wanafanyiwa, lakini wanakaa kimya hivyo ni wajibu wenu kuchukua hatua,” alisisitiza Shekimweri.

Naibu Waziri wa Kilimo na Mbunge wa Dodoma mjini, Antony Mavunde, aliwataka wazazi kuwapa ushirikiano walimu ili kuwasaidia watoto kufanya vizuri katika masomo yao.

“Wazazi tuwape ushirikiano walimu wetu kwani wao ndiyo wanakuwa na watoto wetu kwa muda mrefu tunataka Dodoma kufanya mapinduzi katika sekta ya elimu lazima tuutangaze mkoa wetu kwa ufaulu mzuri hatutaki kuwa Dodoma ile ambayo mtu akiwa na shida ya msichana wa kazi simu ya kwanza anapiga Dodoma na Iringa utamaduni huo lazima ufe mara moja,” alisema Mavunde.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema katika kipindi atakachokuwa mkoani hapo ajenda yake kubwa ni elimu ili kuutoa mkoa katika nafasi za mwisho kitaifa.

“Katika matokeo ya mwaka unaokuja zile nafasi za Dodoma kuwa mkia hapana hatutaruhusu tena na hivi sasa tupo katika mchakato wa kununua mashine kubwa ya kuprinti mitihani print unit ya mkoa ambayo itakuwa na uwezo wa kuchapisha mitihani ya mkoa mzima ili watoto wetu wapate mazoezi ya kutosha,” alisema.

Naye Diwani wa kata hiyo, Dotto Gombo, alisema pamoja na kufanya vizuri katika mtihani wa mwisho wa darasa la saba mwaka jana,wanakabiliwa na tatizo la vyumba vya madarasa.

Gombo, alisema tatizo lingine ni ukosefu wa jengo la ofisi za walimu hali inayosababisha kutumia madarasa ya wanafunzi.




Ofisa Mkuu wa Rasilimali watu wa benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (kulia), akiwasilisha mada kwenye mkutano mkuu wa kitaifa wa wafanyakazi wenye ulemavu nchini, jijini Dodoma juzi. NMB ilikuwa miongoni mwa wadhamini wa mkutano huo uliolenga kujadili upatikanaji wa stahiki bora haki ya kuajiriwa na mazingira rafiki ya kazi kwa watu wenye ulemavu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi wenye ulemavu waainisha matatizo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYAKAZI wenye ulemavu nchini wameainisha baadhi ya matatizo yanayokabili katika maeneo yao ya kazi ikiwamo posho maalumu kwa ajili ya kundi hilo.

Hamisi Hupira, alibainisha hayo wakati akisoma mapendekezo ya matatizo hayo kwa niaba ya wenye ulemavu kwenye mkutano mkuu wa kwanza wa wafanyakazi wenye ulemavu kitaifa uliofanyika jijini hapa jana.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na posho maalumu ya kuwasaidia wafanyakazi hao wenye ulemavu nchini kutokana na mazingira.

Hupira, alitaja matatizo mengine kuwa ni kuomba serikali kuingiza kwenye bima ya afya ununuzi wa vifaa vinavyotumiwa na wenye ulemavu kutokana na aina ya ulemavu.

Alisema serikali iendelee kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye majengo yake yanayojengwa na yaliyopo, kama barabara, vyoo na vifaa maalumu vya kutumiwa na watu weye walemavu.

Aliongeza kuwa bado kuna aina za ubaguzi kwenye maeneo yao ya kazi kama kunyimwa haki za safari kwa kigezo kuwa wana ulemavu.

Matatizo mengi aliyoanisha ni ubaguzi kuhusu ajira kwa sababu kuna baadhi ya ajira wamekuwa wakinyimwa kutokana na ulemavu wao.

Kadhalika, aliomba serikali kusaidia kuweka watoa huduma maalumu kwenye maeneo ya huduma za kijamii kama hospitali, polisi na mahakamani pamoja kuomba serikali kutoa takwimu sahihi za wafanyakazi wenye ulemavu hapa nchini.

Mkurungenzi wa Ikupa Trust, Mbunge wa Viti Maalumu, Stella Ikupa, alisema taasisi yao imesaidia kuwaunganisha wafanyakazi hao na kufanyika kwa mkutano mkuu huo wa kwanza nchini.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kuwaunganisha watu wenye ulemavu ili kujua matatizo yanayowakabili kwenye maeneo yao ya kazi.

“Tumekuwa tukikutana na watu wenye ulemavu maeneo tofauti hapa nchini, lakini leo tumeona tukutane nao wote ili kubaini matatizo yao na kuwasilisha rasmi serikalini,” alisema.

Ikupa alisema anaishukuru serikali kwa kuendelea kutoa ajira kwa watu wenye ulemavu, lakini bado ni chache kulingana na idadi kubwa ya wenye ulemavu wanaohitimu elimu ya juu.

Kwa upande wake mgeni rasmi kwenye mkutano huo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Patrobas Katambi, alisema serikali imechukua matatizo hayo yaliyowasilishwa na watayafanyia kazi.

Katambi alisema serikali imeanza kutangaza nafasi za kazi kwa watu wenye ulemavu kila wanapotangaza ajira mpya.

Kadhalika, alizitaka taasisi kutoa nafasi za kazi kwa watu wenye ulemavu kwa sababu wanauwezo sawa na wengine katika kufanya kazi.

## Ashauri uanzishwaji baraza la watumiaji huduma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI mstaafu wa Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF), Dk. Oscar Kikoyo, ameishauri serikali kuanzisha baraza moja la watumiaji wa huduma kwenye sekta mbalimbali ili kusaidia uchumi wa soko wa Tanzania kubadilika na kuwa imara.

Dk. Kikoyo ambaye pia ni Mbunge wa Muleba Kusini, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye ufunguzi wa mkutano wa wadau wa usafiri wa anga ulioandaliwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huudma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC).

Alisema ni vyema serikali ikawa na mamlaka moja yenye nguvu na sauti kubwa ambayo itawasemea watumiaji wa sekta mbalimbali.

“Uchumi wa soko sio uchumi holela kwani unaendeshwa kwa misingi mitatu ambayo ni mamlaka za udhibiti, mamlaka ya ushindani na mamlaka ya kuwalinda watumiaji, ukiwaacha watoa huduma washindane wenyewe wanaweza kukutana na kupanga hujuma dhidi ya watumiaji.”

“Bahati mbaya hapa Tanzania hatuna mamlaka yenye nguvu ya kuwalinda watumiaji, unapokwenda benki, kuna tozo nyingi, nani anatusemea, na mtumiaji ni kama dampo lakutusemea na kutuelimisha, nchi yoyote ambayo ina mfumo mzuri wa kuwalinda watumiaji uchumi wa soko unakuwa vizuri,” alisema.

Alisema uchumi wa soko imara ni wa watumiaji wanaojua nafasi yao kwenye soko na kutoa taarifa ambazo zinasaidia kuchungulia changamoto zinazojitokeza.

Alisema kuwapo kwa mamlaka ya kuwalinda watumiaji kutaongeza ubunifu, uwajibikaji na kuondoa ukiritimba na uzembe kwa watoa huduma.

Awali, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Innocent Kyara, alisema kwenye mkutano huo kunatarajia maoni yenye kulenga kupata suluhu ya kudumu la kero za watumiaji.

**Alisema ni vyema serikali ikawa na mamlaka moja yenye nguvu na sauti kubwa ambayo itawasemea watumiaji wa sekta mbalimbali.**



HABARI MBEYA

# Madaktari, wauguzi wafunzwa kujikinga na maambukizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADAKTARI na wauguzi 36 wa vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya vya Mkoa wa Mbeya, wamepatiwa mafunzo maalumu ya kujikinga dhidi ya maambukizi (IPC) na namna ya kuhudumia wagonjwa katika hali ya dharura.

Mafunzo hayo yalitolewa juzi na madaktari bingwa kutoka katika hospitali mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam chini ya ufadhili wa Chama cha Watu wenye Kisukari (Tanzania Diabetic Association) na Wizara ya Afya.

Washiriki wa mafunzo hayo walikuwa ni madaktari na wauguzi kutoka katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya pamoja na wa Hospitali ya Mkoa wa Mbeya.

Mratibu wa mafunzo hayo kutoka Chama cha Watu Wenye Kisukari, Dk. Mashombo Mkamba, alisema walianzisha mafunzo hayo wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ambao baada ya kuingia nchini kuliibuka hali ya madaktari kushindwa kuwatofautisha wagonjwa wa ugonjwa huo.

Alisema awali walifanya mafunzo hayo kwa Mkoa wa Dar es Salaam kama eneo la mfano na baadaye wakaamua kusambaza katika mikoa mingine yenye mwingiliano mkubwa wa watu yakiwamo majiji makubwa.

Alisema wakati wa mlipuko wa kwanza wa UVIKO madaktari walikuwa wanashindwa kutofautisha ugonjwa huo na magonjwa mengine ya mfumo wa kupumua hali iliyokuwa inasababisha hata matibabu kuwa hafifu kwenye baadhi ya maeneo.

"Ugonjwa wa UVIKO ulivyoingia ulikuwa wa kutisha kutokana na upya wake na wagonjwa wengi walipoteza maisha, sasa kutokana na hali hiyo hata wahudumu wa afya walikuwa wanaogopa kukalibiana na wagonjwa wenye kufanana na UVIKO na ndiyo maana tukaja na mafunzo haya," alisema Dk. Mkamba.

Mshauri wa masuala ya dharura wa chama cha watu wenye kisukari, Dk. Christopher Mzava, alisema mafunzo hayo yalianza kufanyika katika mikoa mitano ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza kabla ya kuyapeleka mkoani Mbeya.

Alisema mafunzo hayo yana lengo la kuwasaidia wahudumu wa afya na madaktari wanaofanya kazi kwenye vitengo vya dharura kuepuka kupata maambukizi wakati wa kuwahudumia wagonjwa wa dharura.

Alisema lengo la pili ni kuwawezesha wafanyakazi hao kuokoa maisha ya wagonjwa wanaofika katika vituo vyao wakiwa kwenye hali ya umahututi ikiwamo kuwasaidia kupumua kwa kuwaongezea hewa.

"Hapa tulikuwa tunawafundisha hawa madaktari kuwasaidia wagonjwa wetu na ndio maana mmeona tunafanya mpaka mazoezi ya kuwasaidia wagonjwa kupumua, tumewapa mbinu na tumewapa na zana za kufanyia kazi," alisema Dk. Mzava.

Alisema wataalamu waliokuwa wanatoa mafunzo hayo walitoka katika Hospitali ya Taifa Mhimbili, Hospitali ya Mlongazila na Kitengo cha Mifupa cha Hospitali ya Taifa (MOI).

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema mafunzo hayo yaliwasaidia kukumbushwa baadhi ya misingi ya kazi yao hasa katika kuokoa maisha ya watu.

Mmoja wa washiriki hao, Mboka Mwasumbi ambaye ni Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Rungwe alisema kabla ya mafunzo hayo kuna baadhi ya misingi walikuwa wameisahau na wanakusudia kwenda kuwafundisha na wenzao.

Akifunga mafunzo hayo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kuwafundisha wenzao ili kufikia malengo ya waandaaji wa mafunzo hayo ya kuokoa maisha ya watu.



Baadhi ya madaktari na wauguzi wa Halmashauri za Mkoa wa Mbeya, wakifuatilia mafunzo ya kujikinga dhidi ya maambukizi na namna ya kuhudumia wagonjwa katika hali ya dharura, yalitolewa na madaktari bingwa wa hospitali mbalimbali za mkoa wa Dar es Salaam, chini ya ufadhili wa Chama cha Watu Wenye Kisukari na Wizara ya Afya, jijini humo hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watumishi TANROAD watoa misaada maadhimisho Wiki Utumishi wa Umma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Mbeya, wameanza maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kutoa misaada mbalimbali katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Kitengo cha Wazazi Meta ili kuwasaidia wagonjwa na kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa.

Watumishi hao wamefanya usafi katika hospitali hiyo kwa lengo la kuyafanya mazingira kuwa masafi na kufanya wagonjwa wahudumiwe katika mazingira mazuri.

Akizungumza juzi wakati wa kufanya usafi na kutoa msaada huo, Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Nicodemas Kalenzo, alisema waliamua kuanza maadhimisho hayo kwa kuwakumbuka watu wenye uhitaji.

Alisema watumishi wa wakala huo walichangishana fedha kwa ajili ya kununua vitu mbalimbali vya kuwakabidhi wagonjwa na wazazi ambao wamelazwa katika hospitali hiyo ili kuwapunguzia gharama za maisha.

"Watumishi tuliamua kuchangishana fedha na kununua vitu mbalimbali kwa ajili ya kuja kuwasaidia wahitaji walioko kwenye hospitali hii, lakini tumeamua kufanya usafi kuwasaidia kuweka mazingira rafiki zaidi," alisema Mhandisi Kalenzo.

Ofisa Rasilimali Watu Mkuu wa TANROADS, Mkoa wa Mbeya, Safina Mbwelei, alisema walikabidhi mashuka 40 kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa hivyo.

Vilevile, alisema watumishi hao walinunua nguo za kuwasitiri watoto wachanga wanaozaliwa kwenye hospitali hiyo pamoja na sabuni kwa ajili ya kufulia nguo za wagonjwa hasa wazazi.

Watumishi hao pia walinunua maziwa kwa ajili ya watoto ambao wanauhitaji.

"Vifaa vyote tulivyofanyia usafi hapa tutaviacha hapahapa ili viendelee kutumika, nawashukuru viongozi wa hospitali hii kwa kuturuhusu kuja kufanya kazi hii hapa," alisema Safina.

Akizungumza kwa niaba ya uongozi wa hospitali hiyo, Judica Minja, aliwashukuru watumishi wa wakala huo kwa kuwasaidia wagonjwa kwenye hospitali hiyo na akaahidi vitu vyote vitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema misaada hiyo itawasaidia kuwahudumia wagonjwa ambao hawana msaada wa ndugu wa karibu na kuwaomba waendelee kuwa na moyo wa kusaidia wahitaji.

Hospitali hiyo, alisema ina wagonjwa ambao wakati mwingine wanakosa msaada wa karibu kutokana na sababu mbalimbali na kuifanya kuwa na mzigo mkubwa.

"Kwa niaba ya uongozi wa hospitali hii nawashukuru sana kwa misaada yenu na ninawaahidi kwamba tutawafikishia walengwa ili iwasaidie na nitafikisha salamu zenu kwao, Mungu awabariki sana," alisema Judica.

Hospitali hiyo inahudumia wagonjwa kutoka katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na baadhi wa kutoka nchi jirani.

# Viongozi waonywa kupokea fedha za wachimbaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa vijiji wanaogawa maeneo ya uchimbaji madini katika Wilaya ya Chunya kwa kupokea fedha kwa baadhi ya wachimbaji, wametakiwa kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa inasababisha migogoro miongoni mwa wachimbaji.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, alitoa tahadhari hiyo juzi alipokuwa anafungua kongamano la siku mbili la madini na nishati la mkoa huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Juma Homera na kusema serikali itaanza kuwachukulia hatua.

Mayeka alisema tatizo hilo ni miongoni mwa mambo yanayoifanya sekta ya madini katika wilaya hiyo kushindwa kukua na hata wananchi kutonufaika na madini hayo ambayo ni miongoni mwa rasilimali kubwa katika wilaya hiyo.

"Kuna hili tatizo la utoroshaji wa madini, tunaendelea kupambana na tatizo hili kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta hii ili kukomesha tatizo hili," alisema Mayeka.

Aliwataka wachimbaji wa madini kuhakikisha wanauza madini hayo kwenye masoko yaliyoainishwa na serikali ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria.

Alisema mtu yeyote anayekamatwa akitorosha madini hatua ya kwanza serikali inataifisha madini hayo na kumchukulia hatua zingine za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Alisema kwa sasa kutokana na kukua kwa teknolojia, bei ya dhahabu inajulikana katika soko la dunia na wachimbaji wanatakiwa kabla hawajauza dhahabu zao wafuatilie kwanza bei ya soko la dunia.

Baadhi ya wachimbaji wa dhahabu waliiomba serikali kuwasogezea baadhi ya huduma kwenye maeneo yao ili kuwapunguzia gharama za uendeshaji wa shughuli zao.

Mmoja wa wachimbaji hao, Njunjuru Mhewa, alisema baadhi ya huduma muhimu zikiwamo maabara za kupimia kiwango cha dhahabu zipo Dodoma hali inayowafanya watumie fedha nyingi kwenda kufuata huduma hizo.



## Wazazi wabanwa kukwepa ushahidi wa kesi za ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Awadh Juma Haji, amelitaka jeshi hilo kuwafungulia mashtaka wazazi ambao hawapo tayari kutoa ushahidi mahakamani baada ya watoto wao kufikisha malalamiko ya kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Amesema tabia ya wazazi kukwepa kutoa ushahidi mahakamani imekuwa ikisababisha kesi hizo kulazimika kufutwa.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea mikoa miwili ya Pemba kuangalia utendaji kazi wa Jeshi la Polisi katika kukabiliana na matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, zikiwamo kesi za matukio ya ubakaji.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga kuzipatia ufumbuzi kesi za udhalilishaji wa kijinsia zinazofikishwa mahakamani kwa kufanyiwa kazi.

Kamishna huyo alisema kumejitokeza tatizo kubwa la wananchi kukataa kutoa ushahidi mbele ya vyombo vya sheria, ikiwamo mahakamani na matokeo yake kesi hizo kufutwa.

"Ninaliagiza Jeshi la Polisi Pemba kuwatafuta watu wote wanaokataa kutoa ushahidi mahakamani na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria kwa sababu wanakwenda kinyume cha mikakati ya serikali ya kushughulikia kesi hizo kwa haraka," aliagiza.

Vilevile, aliwaagiza watendaji wa Jeshi la Polisi katika kikosi cha upelelezi kuharakisha kukamilisha kazi ya kuchunguza mwenendo wa kasi kwa ajili ya kufikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na kutajwa.

Alisema miongoni mwa malalamiko yanayotolewa na wananchi ni Jeshi la Polisi kuchelewa kukamilisha ushahidi wa matukio ya kesi hizo kwa ajili ya kutajwa mahakamani, matokeo yake wananchi hukata tamaa na wengine kuamua kuacha kufika mahakamani, hivyo kesi hizo hulazimika kufutwa na mahakama kutokana na kukosa ushahidi.

"Jeshi la Polisi tunalalamikiwa sana kwamba tunachelewesha kukamilisha upelelezi wa mashauri ya kesi za udhalilishaji wa kijinsia na wananchi kukata tamaa," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alisema muhali unapelekea wananchi kukataa kutoa ushahidi na wakati mwingine kufuta kesi ni sehemu ya shida kubwa zinazokwamisha upelelezi wa matukio hayo.

"Tunakabiliwa na muhali katika utekelezaji wa majukumu yetu ikiwamo katika kukamilisha upelelezi, wananchi hawapo tayari na wakati mwingine wanasuluhisha kesi hizo kienyeji au unakuta tayari wamekubaliana kufunga ndoa," alisema.

Jaji wa Mahakama Kuu Pemba, Ibrahim Mohamed, alisema wameongeza kasi ya kusikiliza mashauri mbalimbali yanayofikishwa kwao ikiwamo ya udhalilishaji wa kijinsia.

# Mwinyi apongeza mfuko kuimarisha sekta muhimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameushukuru Mfuko wa Misaada wa Sheikh Zayed bin Sultan Al Nahyan kwa kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta za afya, elimu na ustawi wa jamii.

Dk. Mwinyi alitoa shukrani hizo jana Ikulu Zanzibar baada ya kushuhudia utiaji saini kati ya serikali yake na mfuko huo kutoka nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), mfuko ukisaidia katika sekta za elimu, afya na ustawi wa jamii.

Alisema mfuko huo umechukua uamuzi stahiki wa kuisaidia Zanzibar katika maendeleo yake ikiwa ni pamoja na azma ya kujenga shule mbili, kituo cha wazee cha kisasa na hospitali.

Alisema hatua hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendeleza ujenzi wa miradi ya maendeleo unaotekelezwa hivi sasa.

Rais Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kutoa shukrani kwa Rais wa UAE, Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha miradi ya maendeleo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema mfuko huo una azma ya kujenga shule mbili za Muembeladu na Mtopepo, kituo cha kisasa cha wazee kitakachokuwa na nyumba za watendaji wake pamoja na kujenga hospitali ya kisasa.

Waziri Mkuya alisema kuwa nchi za UAE zina uhusiano mzuri na Zanzibar, hivyo hatua hiyo itasaidia utekelezaji wa mikakati katika maeneo aliyoyapa kipaumbele Rais Dk. Mwinyi. Aliahidi wizara yake itahakikisha inatoa ushirikiano mkubwa kwa taasisi hiyo ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Mkuu wa Taasisi hiyo, Sheikh Hamad Salem bin Kardous Al Amer, alisema UAE ina uhusiano mwema na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwamo Zanzibar.

Alisema kuwa misaada hiyo ni hatua za kiongozi mkuu wa nchi hiyo katika kuiunga mkono Zanzibar na anatambua uhusiano na ushirikiano uliopo ambao kuna haja ya kuendelezwa na kudumishwa.

Kiongozi huyo alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa hatua zake za kuendeleza uhusiano na ushirikiano mwema kati ya Zanzibar na UAE sambamba na ukarimu mkubwa alionao kwa nchi za umoja huo.

Aliongeza kuwa hatua hiyo pia itasaidia kuanzisha ziara kati ya pande mbili hizo zitakazosaidia kuimarisha uhusiano na ushirikiano mkubwa ulioko huku akimwomba Mwenyezi Mungu kuipa Zanzibar maendeleo makubwa yenye amani ndani yake.

Utiaji saini ulishuhudiwa na Rais Dk. Mwinyi kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mfuko wa Misaada wa Sheikh Zayed bin Sultan Al Nahyan, upande wa serikali ukiwakilishwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akil na upande wa mfuko huo ukiwakilishwa na na Sheikh Hamad Salem bin Kardous Al Amer.



Daktari wa Kituo cha Afya Mpendae Unguja, Hamad Khamis Ali (kulia), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri Wizara ya Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, kuhusiana na utendaji wa kazi katika kituo hicho, alipofanya ziara ya kikazi, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri awapa angalizo wauguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, amewataka wauguzi wanaoshughulikia miradi mbalimbali kurudi katika vituo vya afya ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Alitoa agizo hilo jana katika ziara ya kuangalia utendaji kazi kwa vituo vya afya vinavyotoa huduma ya mama na mtoto katika kituo cha afya Mpendae na Sebleni Wilaya ya Mjini Unguja.

Naibu Waziri huyo alisema kurudi kwa wauguzi hao kutasaidia kuondoa usumbufu uliopo katika vituo hivyo katika kupata huduma.

Alisema amegundua changamoto nyingi ikiwamo uchelewaji wa watendaji wa afya, hali inayopelekea wananchi kusubiri muda mrefu kupata huduma. Hassan alieleza kuwa azma ya serikali ni kuwapatia wananchi huduma bora, hivyo watendaji wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na kufuata sheria za kazi ili kuondosha usumbufu kwa wagonjwa wanaofika vituoni kupata huduma.

Alisema wizara haitosita kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaokiuka majukumu yao na kusababisha uzoroteshaji wa huduma hiyo ili kuepusha malalamiko kwa jamii.

Naibu Mkurugenzi wa Kinga Wizara ya Afya, Salim Slim, alisisitiza ushirikiano katika malezi kwa kina baba kuwapeleka watoto kliniki ili kujua maendeleo ya ukuaji wa afya za watoto wao.

Baadhi ya watendaji wa vituo hivyo walisema wanakabiliwa na vikwazo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vipimo vya damu kwa mama wajawazito na gari la kubeba wagonjwa wa dharura.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALIMU OMARI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0924-0046** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **IKUNGI** mwaka **2002,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa TBT/L/R/I/VOL2/1/6/2016**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK ANTHONY NYANZWERI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.938/106/2003** kilichotolewa na **BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA** kupitia shule ya **MBEZI BEACH HIGH SCHOOL.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI CONTROL NAMBA: 9910833382551**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAYMOND TEEKISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye namba za usajili **T226 CET**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**

**ARU/ARU/RB/253689/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 507 CEH**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa**

**ARU/ARU/RB/253802/20**

## KUPOTEA KWA HATI ZA KUMILIKI VIWANJA

**NDUGU AYUTO VITUS KALIMUWABU** anatangaza kupotelewa na hati za viwanja **PLOT NO. 595 NA 596 BLOCK C** Eneo IYUMBU WEST HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake.

**Taarifa ya Polisi**

**DOD/DOD/RB/250736/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya IYUNGA**
**Wilaya ya MBEYA**
**MADAI NAMBARI 41/2022 YA.........**
**Mdai: FRANSISCO JAILOS KAOMBWE**
**Mdaiwa: EZEBIUS V. SANGA**
**Kwa: EZEBIUS V. SANGA**
**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**NI JUU YA GARI AINA YA NISSAN HARD NAMBA T. 111 BAV**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama siku ya tarehe 4/7/2022 saa 2:30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na shauri hilo kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hali zote zinazohusu shauri hilo kwa njia ya kujitetea katika shauri hili. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shauri hili litaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21/6/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 19 YA 2022**
**PERUZ BALALUGILA.....................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**FROLA MALINGULA................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA FROLA MALINGULA**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe **20/07/2022** mbele ya Mwenyekiti M.Khassimu wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 28.06.2022.

**M. KHASIM**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**KISIMBO EMMANUEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S101/253** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **AZANIA** mwaka **1993** ,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa UD/RB/1051/2001**

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Wahamiaji 46 wafariki wakiingia Marekani

**TEXAS,** Marekani

MIILI ya watu 46 imepatikana baada ya kutelekezwa kwenye trela la lori katika barabara ya mji wa San Antonio, Jimbo la Texas nchini Marekani.

Vifo vya watu hao vinaelezwa na mamlaka ya eneo hilo kuwa ni tukio la usafirishaji wa wahamiaji ulioshindwa kufanikiwa.

Maofisa wamesema watu wengine 16 wamepelekwa hospitali wakiwamo watoto wanne.

Mkuu wa Polisi Willian McManus, alisema mfanyakazi wa baraza la mji huo ndiye aliyegundua miili hiyo.

Meya wa Mji wa San Antonio, Ron Nirenberg, alielezea kisa hicho kama janga, na kuongeza kuwa watu hao waliofariki ni familia ambazo zilikuwa zinajaribu kutafuta maisha bora.

Tukio hilo linatajwa kuwa miongoni mwa mikasa mibaya kuwahi kushuhudiwa nchini humo kwa watu wanaojaribu kuvuka mpaka wa Mexico na kuingia Marekani kinyume cha sheria.

Mwaka 2017, wahamiaji 10 walikufa baada ya kukwama ndani ya lori lililokuwa limeegeshwa katika duka moja mjini San Antonio. **DW**

## Wabunge Israel waidhinisha kulivunja bunge

**TELI AVIV,** Israel

WABUNGE wa Israel kwa kauli moja wameidhinisha muswada wa kulivunja bunge.

Hatua hiyo muhimu ya kisheria inaisukuma nchi hiyo kuelekea uchaguzi wake wa tano katika muda wa chini ya miaka minne.

Tangu wiki iliyopita, wabunge wa muungano wa Waziri Mkuu anayemaliza muda wake Naftali Bennett na upinzani unaoongozwa na Waziri Mkuu wa zamani Benjamin Netanyahu, wamekuwa wakizozana bungeni juu ya muswada wa kulivunja bunge hilo la Knesset.

Muungano huo ulisema ulitaka kuidhinishwa haraka kwa muswada huo baada ya Bennett kutangaza wiki iliyopita kwamba muungano wake wa vyama vinane uliogawika hauwezi tena kudumu.

Hata hivyo Netanyahu na washirika wake wamekuwa wakifanya mazungumzo ya kutaka kuunda serikali mpya inayoongozwa na Netanyahu katika bunge la sasa, hatua ambayo ingeepusha kufanyika kwa uchaguzi mpya.

Utayari wa upinzani kulivunja bunge unaonyesha kuwa juhudi za Netanyahu za kuunda serikali mpya zimekwama. **DW**

# Russia yataka Ukraine kujisalimisha kumaliza vita

**MOSCOW,** Russia

RUSSIA imesema itamaliza mashambulizi dhidi ya Ukraine, kama serikali ya nchi hiyo na majeshi yake itakapojisalimisha.

Alizungumza na vyombo vya habari, msemaji wa serikali ya Russia, Dmitry Peskov, aliitaka serikali ya nchi hiyo kuamuru wanajeshi wao kuweka silaha chini.

"Upande wa Ukraine unaweza kusimamisha kila kitu kabla ya mwisho wa leo (jana)," Peskov alisema, kulingana na shirika la habari la Agence France-Presse.

Alisisitiza "Amri kwa vitengo vya wanajeshi kuweka chini silaha zao ni muhimu."

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alisema mara kwa mara kuwa wanajeshi wa nchi yake hawatasalimu amri na kwamba watakuwa washindi katika vita hivyo.

Hata hivyo, juzi aliwaambia viongozi wa nchi tajiri duniani wa G7, kuwa anatamani vita vimalizike mwishoni mwa mwaka huu kabla ya kuingia majira ya baridi kwa sababu wanajeshi wake hawatakuwa na uwezo wa kupambana.

Katika hatua nyingine viongozi wa Ulaya wanatarajiwa kukutana mjini Madrid nchini Hispania katika mkutano wa NATO, ambao wanalenga kuidhinisha mipango ya kuongeza idadi ya wanajeshi walio katika hali ya tahadhari hadi kufikia 300,000.

**mashambulizi ya makombora katika eneo la Kremenchuk yamelifanya taifa la Russia kuwa sawa na shirika kubwa la kigaidi zaidi duniani.**

Peskov, alielezea NATO kama kambi yenye fujo iliyoundwa kwa makabiliano.

Msemaji huyo alieleza kwamba mashambulizi dhidi ya Ukraine yataendelea hadi kufikia malengo yake.

### MAKOMBORA YALIPUA KITUO CHA BIASHARA

Wakati huo huo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kumaliza ugaidi wa Russia, baada ya makombora kuteketeza kituo cha biashara.

Alisema mashambulizi ya makombora katika eneo la Kremenchuk yamelifanya taifa la Russia kuwa sawa na shirika kubwa la kigaidi zaidi duniani.

Kufikia sasa, watu 18 wanakisiwa kuuawa na wengine kujeruhiwa katika tukio hilo.

Zelensky alionya kuwa kunaweza kuwa na zaidi ya watu waliouawa kutokana na uokoaji wa watu waliofukiwa kwenye kifusi unaendelea.

### RUSSIA YAJIANDAA KUSHAMBULIA SLOYANSK

Wanajeshi wa Russia wanatengeneza mazingira ya kuishambulia Slavyansk.

Harakati hizo zinaonyesha zimejikita katika kuendeleza mashambulizi kuelekea Izyum na Slavyansk.

### G7 YAAHIDI MSAADA WA KIFEDHA KUKABILIANA NA MGOGORO WA CHAKULA DUNIANI

Kundi la mataifa saba yaliyostawi zaidi kiviwanda duniani (G7) linatarajia kuhitimisha mkutano wake wa kilele kwa kutoa ahadi ya kifedha kuelekea juhudi za kukabiliana na mgogoro wa chakula duniani.

Tatizo la upungufu wa chakula duniani linachochewa na vita vya nchini Ukraine.

Viongozi wa Uingereza, Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan na Marekani walitoa tamko la pamoja juu ya maendeleo yaliyopatikana katika mkutano huo uliofanyika katika hoteli ya Schloss Elmau hapa Ujerumani.

Viongozi hao wa G7 pia wametoa ishara ya mshikamano dhidi ya Russia ikiwamo kupunguza utegemezi wa nishati kutoka nchini humo na kuiwekea vikwazo. **BBC**



Barakatullah akiwa kwenye mlango wa nyumba yake ambayo iliharibiwa na tetemeko la ardhi wiki iliyopita katika kijiji cha Spera Wilaya ya Khost nchini Afghanistan. **PICHA: REUTERS**

# Wauguzi 19 wa Kenya wapata ajira Uingereza

**NAIROBI,** Kenya

WAZIRI wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, amewaaga kundi la wauguzi 19 ambao wanakwenda kufanya kazi nchini Uingereza.

Kuajiriwa kwa wauguzi hao inatokana na makubaliano ya pande mbili kati ya Kenya na Uingereza yaliyofikiwa na Rais Uhuru Kenyatta na Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, Julai mwaka jana.

Kagwe alisema kuwa mchakato mkali ulifanywa ili kupata orodha ya mwisho kutoka kwa wauguzi 3,329 waliotuma maombi mwaka jana.

Kati ya 19 waliohitimu, 13 wataambatanishwa na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Oxford na wataondoka nchini humo Juni 28. Sita waliosalia bado haijafahamika sehemu zao za kazi na watasafiri Uingereza baada ya wiki mbili.

Aidha, wauguzi 80 waliohitimu ambao watakuwa sehemu ya kundi la pili.

Kagwe aliwataka wauguzi wengine pia kuangalia fursa kama hizo na kutuma maombi.

"Wahudumu wa afya wa Kenya wanapaswa kuwa na mawazo mapana. Ukweli kwamba ulifunzwa nchini Kenya haupaswi kukuweka nchini pekee. Fikiri kwa mapana na utafute fursa nje ya nchi." Alisema.

Alirejelea kusema kuwa Kenya kuwa kitovu cha utalii wa afya akisema kuwa kuajiriwa wauguzi hao nchini Uingereza kunaonyesha ubora wa mafunzo yaliyotolewa na taasisi za ndani nchini humo. **BBC**

# PRISONS KWENYE MTIHANI MZITO

**Na Cheji Bakari,** TANGA

KOCHA msaidizi wa timu ya Tanzania Prisons, Shabani Mtupa amesema kuwa mechi yao ya leo dhidi ya Ruvu Shooting anaiona ni fainali ngumu kwa upande wao kutokana na nafasi waliyokuwepo katika msimamo wa Ligi Kuu.

Prisons na Ruvu Shooting watacheza mechi ya mwisho ya kumaliza Ligi Kuu Bara katika uwanja wa Mabatini, Mlandizi Pwani.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara timu ya Ruvu Shooting ipo katika nafasi ya 13 ikiwa na alama 31 wakati Prisons wapo nafasi ya 14 wakiwa na alama 29.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu kutokea Kibaha mkoani Pwani, Mtupa alisema kuwa ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya Simba umewapa morali wachezaji kuelekea mechi ya mwisho dhidi ya Ruvu Shooting, lakini kwa upande wao wanaona mechi hiyo ni ngumu zaidi.

"Hii mechi itakuwa ngumu sana kwa upande wetu kutokana na kuwa kila timu inahitaji matokeo mazuri ili ibaki Ligi Kuu kutokana na nafasi zetu katika msimamo wa Ligi tulipokuwepo".

"Hivyo nguvu zote tunazielekeza katika mechi hii ili tupate matokeo mazuri na tujihakikishie usalama wa kubaki ligi kuu msimu ujao."



Msanii wa sarakasi, Hassan Jogan 'Rosalinyo', akionyesha mbwembwe zake katika tamasha la Zege Day lililofanyika katika viwanja vya Mwembeyanga Temeke Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam kuboresha zaidi kikosi*

**Na Saada Akida**

KLABU ya Azam msimu huu haikuwa na mwenendo mzuri huku wakiwa na presha kuwania nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi hiyo inayomalizika leo, kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat'

Akizungumza na gazeti hili Popat alisema hawakuwa na msimu bora kwa sababu malengo yao yalikuwa kutwaa ubingwa au kumaliza katika nafasi ya pili ya msimamo jambo ambalo hawajafanikiwa. Alisema kwa sababu ya matokeo ya msimu huu wanalazimika kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi kulingana na ripoti ya benchi lao la ufundi.

"Tunasubiri ripoti ya mwalimu, msimu umemalizika tutaona ni wapi tunapaswa kufanya maboresho, wachezaji gani tunatakiwa kuwaongeza kikosini, watakaotolewa kwa mkopo na ambao tutawaacha kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili," alisema Popat. "Usajili wetu utazingatia mahitaji ya benchi la ufundi kwa kiasi kikubwa na hatutasajili kwa mbwembwe kama wenzetu wanavyofanya, kikubwa mashabiki wetu wawe watulivu msimu ujao tunakuja tukiwa imara zaidi," aliongeza.

Alisema usajili huo unalinganaa na mikakati yao ya msimu ujao kuwa bora zaidi na kufanikiwa hilo wanatakiwa kufanya usajili wa wachezaji wenye kiwango bora na kuleta ushindani mkubwa.

Kikosi cha Azam kitakuwa nyumbani leo kuwakaribisha Biashara United katika mchezo wa Ligi hiyo mchezo utakaopigwa katika uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi.

## Coastal kazi moja tu kwa Geita Gold

**Na Cheji Bakari,** TANGA

BAADA ya kupoteza mchezo dhidi ya Kagera Sugar, Coastal Union sasa inajipanga kumalizia vizuri mechi ya mwisho dhidi ya Geita Gold FC ili iondoke na ushindi leo.

Katika mechi iliyopita iliyochezwa katika uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Kagera Sugar walitibua mipango ya Coastal ya kutaka ushindi ili imalize Ligi Kuu ikiwa katika nafasi nne za juu.

Akizungumza na gazeti hili mara baada ya mazoezi ya asubuhi katika viwanja vya Popatlal jijini Tanga, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema kuwa amefanya kikao na wachezaji wake ili kuziba mapungufu yaliyojitokeza kuelekea mechi dhidi ya Geita Gold.

"Nimetoka mazoezini nipo kwenye kikao na wachezaji wangu kupeana mawili matatu kuelekea mechi ya Geita Gold FC," alisema.

Kwa upande wake msemaji wa timu hiyo, Miraji Wandi alisema kuwa katika mechi iliyopita dhidi ya Kagera Sugar, kikosi cha Coastal kilionesha uwezo mkubwa lakini kwa upande wa Kagera Sugar walitumia vema nafasi waliyoipata na kuibuka na ushindi huo.

"Kama unavyojua wachezaji wetu walijitahidi vya kutosha lakini bahati haikuwa upande wetu."

## Timu ya Cabbadi kuingia kambini Z'bar

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Cabbadi yenye wachezaji 24 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, inatarajiwa kuingia kambini Julai 4 mwaka huu kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika yatakayoanza kutimua vumbi Julai 22 hadi 29 nchini Misri.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana Mwenyekiti wa Chama cha mchezo huo Tanzania (TCA), Abdalah Nyoni alisema lengo la mashindano hayo ni kupata bingwa wa Afrika pamoja na timu tatu zitakazokwenda kushiriki Kombe la Dunia mwishoni mwa Oktoba mwaka huu nchini India.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi ya Cameroon, Nigeria, Algeria, Ghana, Tanzania, Kenya pamoja na wenyeji wa mashindano Misri.

Alisema maandalizi kwa upande wa Tanzania yanaendelea huku kila mchezaji akiahidi kwenda kufanya vizuri ili kuiwakilisha vema nchi ya Tanzania.

"Tumeamua kuweka kambi mapema ili turekebishe makosa madogo madogo yasiende kujitokeza kwenye mashindano hayo tunataka tukaitangaze nchi yetu," alisema Nyoni.

Alisema droo ya mashindano hayo itachezeshwa Julai 16 mwaka huu ambapo itawaonesha wamepangwa kundi gani na nani wanakwenda kuanza nao.

Alisema anaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuwaunga mkono ili wafanikishe safari yao ambayo wanatarajia kuondoka hapa nchini Julai 21 mwaka huu kuelekea nchini humo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICHARLISON ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Richarlison, 25, na winga wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21 kutoka Everton. ***(Sky Sports)***

### GORDON HAUZWI

EVERTON haina nia ya kumuuza Anthony Gordon ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Goodison Park unakamilika mwaka 2025. ***(Liverpool Echo)***

### LENGLET AWINDWA

TOTTENHAM Hotspur pia wana nia ya kumsajili beki wa Barcelona na Ufaransa, Clement Lenglet, 27, licha ya AS Roma kuwa na nia ya kumsajili mchezaji huyo. ***(London Evening Standard)***

### BELLINGHAM AWANIWA

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham, 18, atakuwa mchezaji anayesakwa sana na Real Madrid msimu ujao, licha ya kwamba klabu hiyo ya Hispania inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea na Liverpool. ***(AS, via Mail)***

### CHELSEA YATAFUTA BEKI

BAADA ya kufungua mazungumzo na klabu ya Manchester City kuhusu kumsajili Raheem Sterling, 27, Chelsea inajaribu pia kutafuta beki. ***(Telegraph)***

### SALAH KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 30, anatarajiwa kuondoka mwisho wa msimu wa 2022-23 akiwa mchezaji huru. Salah amefunga mabao 156 katika mechi 254 tangu alipojiunga na Wekundu hao mwaka 2017. ***(Mirror)***

### MARTINEZ ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wamewasilisha ofa ya pauni milioni 35 kwa mlinzi wa Ajax, Lisandro Martinez, 24, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Argentina. ***(Mirror)***

### MAN NA JONG

KLABU ya Manchester United ina matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, 25. ***(Mirror***

### BOTMAN ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inatazamia kukamilisha usajili wa pauni milioni 32 wa mlinzi wa Lille, Sven Botman, 22. ***(Mail)***

### GALTIER KUINOA PSG

CHRISTOPHE Galtier, ambaye aliiongoza Nice msimu uliopita, anakaribia kuteuliwa kuwa kocha mpya wa Paris St-Germain, huku Mauricio Pochettino akitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo licha ya kushinda taji la ligi. ***(ESPN)***

### DEMBELE BASI TENA

BARCELONA hawataboresha ofa yao ya mkataba kwa mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 25, ambaye mkataba wake na timu hiyo ya LaLiga unamalizika kesho. Mchezaji huyo ana ofa kutoka kwa Bayern Munich, Chelsea na PSG. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA WAMFUATA RAHEEM STERLING

**LONDON,** England

### ●●● Wafanya mazungumzo ya kumtaka Stamford Bridge, mwenyewe asita..

CHELSEA wamefanya mawasiliano na Manchester City kuhusu Raheem Sterling lakini bado hajathibitisha ni wapi anataka kucheza soka lake msimu ujao, kwa mujibu wa 90min.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 mkataba wake unamalizika 2023 na amepewa ofa ya mkataba mpya wa muda mrefu pale Uwanja wa Etihad, lakini bado hajaipa City majibu ya uhakika.**

Kwa hali ilivyo, Sterling ana chaguzi tatu; kubaki Man City kwa muda mrefu, kuondoka msimu huu wa joto au kubaki hadi msimu ujao wa joto na kisha kuondoka kwa uhamisho wa bure.

Sterling anaaminika kufikiria kila chaguo, lakini Chelsea wanafanya msukumo madhubuti na wanampa njia ya kuondoka City msimu huu wa joto.

Vyanzo vya habari vimethibitisha kwamba, Sterling hayuko wazi kuhusu mustakabali wake na 'alisikitishwa' kuhusu kuachwa kwenye benchi kwa baadhi ya michezo muhimu - ikiwa ni pamoja na mechi ya pili ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid.

Sterling anafikiria sana kuondoka kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa joto kwani anajua chaguzi zake zitakuwa nyingi.

Hajawahi kuficha hamu yake ya kucheza nje ya nchi, na Barcelona na Real Madrid zinatajwa kuwa ndio timu anazoziwania.

"Tangu nikiwa mtoto, asilimia 100 imekuwa ndoto yangu kucheza nje ya nchi mahali fulani. Ingekuwa vizuri siku moja kumaliza mazoezi na kurudi nyumbani na kukaa kwenye bustani yako na kula chakula cha jioni," alisema mwaka 2019.

Hata hivyo, Chelsea wameweka wazi kwa City na Sterling kwamba wanataka dili mara moja.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,010,68
MECHI KALI
AZAM
VERSUS
BIASHARA UNITED
1 | 2.02
X | 2.99
2 | 3.68
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ORIGI ATUA RASMI MILAN

**MILAN,** Italia

DIVOCK Origi amepigwa picha akiwa jijini Milan akijiandaa kukamilisha uhamisho wa kujiunga na wababe hao wa Italia kutoka Liverpool.

Mkataba wa mshambuliaji huyo unaisha mwishoni mwa mwezi huu na anatazamiwa kujiunga na Rossoneri hao kwa uhamisho wa bure.

Kama ilivyoripotiwa na 90min, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifikia makubaliano ya maslahi binafsi na washindi hao wa Serie A, Mei mwaka huu, akikataa ofa kutoka kwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England.

Zaidi ya mwezi mmoja baadaye, Origi sasa amesafiri hadi Milan kukamilisha uhamisho wake.

Mwandishi wa habari wa Italia, Daniele Longo alishiriki video ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akitoka kwenye uwanja wa ndege wa jiji hilo na kupiga picha Jumatatu jioni.

Origi alikuwa amepewa ofa mpya na Liverpool lakini akakataa huku akitafuta soka la kucheza kikosi cha kwanza.

Mbelgiji huyo mara nyingi amekuwa sio mchezaji chaguo la kwanza kwa kocha, Jurgen Klopp, akianza chini ya michezo 40 katika muda wake pale Anfield.

# *Lewandowski ni suala la muda tu Barcelona*

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas amekiri angependa kuidhinisha uhamisho wa Barcelona kumnunua Robert Lewandowski, lakini shughuli hiyo inategemea kama Blaugrana hao watakidhi 'vigezo' vya kiuchumi katika siku chache zijazo.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta aliongoza mkutano wa wanachama wa Klabu hiyo wiki iliyopita ambapo alifichua mpango wa kurudisha nguvu za kiuchumi ambazo zitasaidia kupunguza upotevu wa kifedha ulitokea msimu wa 2021/22 na kuwawezesha kufanya usajili wa fedha nyingi msimu huu wa joto.

Mlengwa namba moja wa Barca bado ni Lewandowski, ambaye mwezi uliopita alisema hadharani kuwasihi Bayern Munich kumruhusu kuhamia Katalunya kabla ya mkataba wake kumalizika mwaka ujao.

Tebas, mkosoaji anayejulikana wa shughuli za kifedha za Barcelona katika miaka michache iliyopita, amekiri kuwa angeidhinisha dili la Lewandowski ikiwa ni muhimu kwa klabu hiyo.

"Ninatumaini kwamba Lewandowski atachezea Barcelona na ana msimu mzuri. Ninatumaini kwamba, wale wawezeshaji wa kifedha ambao Laporta anawatumia watamfikisha Barcelona, kwa sababu ni gwiji wa Bayern Munich na soka la Ulaya," alisema Tebas.



89,585/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.7.2022 | 22:00 | Ituano SP vs Criciuma SC | 2.41 | 2.93 | 3.18 |
| 2.7.2022 | 22:30 | Fluminense vs Corinthians | 2.23 | 3.04 | 3.48 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Santos vs Flamengo | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 3.7.2022 | 01:00 | Ceara CE vs Internacional | 2.49 | 3.04 | 2.99 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Toronto vs Seattle Sounders | 2.65 | 3.75 | 2.43 |
| 3.7.2022 | 02:30 | CRB AL vs Guarani SP | 2.39 | 2.82 | 3.37 |
| 3.7.2022 | 02:30 | Gimnasia y Esgrima vs Defensa Justicia | 2.27 | 3.39 | 3.19 |
| 3.7.2022 | 13:30 | Suwon Samsung vs Incheon Utd | 2.49 | 3.19 | 2.89 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Varbergs Bois vs IFK Varnamo | 2.49 | 3.15 | 2.90 |
| 3.7.2022 | 16:00 | Djurgardens IF vs Hammarby | 2.23 | 3.42 | 3.08 |
| 3.7.2022 | 18:00 | Danubio FC vs River Plate (URU) | 2.52 | 3.16 | 2.81 |
| 3.7.2022 | 18:30 | BK Hacken vs Elfsborg | 2.41 | 3.52 | 2.73 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Union Santa Fe vs Lanus | 2.25 | 3.20 | 3.30 |
| 3.7.2022 | 19:00 | Aalesunds vs Stromsgodset | 2.24 | 3.47 | 3.02 |
| 3.7.2022 | 21:00 | Barracas Central vs San Lorenzo | 2.90 | 3.15 | 2.50 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.99 | 3.04 | 2.48 |
| 3.7.2022 | 22:00 | Bahia BA vs Gremio | 2.63 | 2.78 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 29/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1198 | Adelaide Olympic vs Adelaide Utd Youth | 1.81 | 3.83 | 3.49 |
| 14:30 | 2878 | Changchun Yatai vs Hangzhou NG | 2.21 | 3.19 | 2.99 |
| 14:45 | 3256 | Lion City Sailors vs Young Lions | 1.07 | 8.87 | 17.74 |
| 15:00 | 3633 | Yassi Turkistan vs FC Zhetysu | 3.95 | 3.45 | 1.85 |
| 16:00 | 1500 | Kaisar Kyzylorda vs Zhenis Nur-Sultan | 1.24 | 5.32 | 9.45 |
| 16:00 | 2367 | Terengganu vs Negeri Sembilan | 1.60 | 3.85 | 5.20 |
| 16:00 | 3303 | Mbeya Kwanza FC vs Simba | 5.12 | 3.30 | 1.66 |
| 16:00 | 4313 | Kagera Sugar vs Polisi Tanzania | 2.16 | 2.70 | 3.74 |
| 16:00 | 4463 | Sidama Bunna SC vs Hadiya Hosahina FC | 2.45 | 2.79 | 2.99 |
| 16:00 | 4868 | Young Africans vs Mtibwa Sugar | 1.48 | 3.74 | 6.29 |
| 16:00 | 5213 | Azam vs Biashara United | 2.02 | 2.99 | 3.68 |
| 16:00 | 5292 | Ruvu Shooting vs Tanzania Prisons | 2.26 | 2.70 | 3.49 |
| 16:00 | 5926 | Mbeya City vs Namungo | 2.17 | 2.75 | 3.63 |
| 16:30 | 3888 | Poland W vs Iceland W | 3.69 | 3.59 | 1.82 |
| 17:00 | 5577 | FC Gagra vs Saburtalo Tbilisi | 2.84 | 3.28 | 2.26 |
| 17:30 | 5695 | Tammeka Tartu vs Trans Narva | 2.37 | 3.65 | 2.60 |
| 18:00 | 1005 | Inter Turku vs HJK Helsinki | 2.94 | 3.19 | 2.24 |
| 18:00 | 3081 | Pakhtakor vs Bunyodkor | 1.35 | 4.70 | 8.00 |
| 18:00 | 4975 | BATE Borisov vs Slutsk | 1.32 | 4.71 | 7.85 |
| 18:00 | 5474 | Surkhon Termez vs Neftchi Fargona | 2.45 | 2.90 | 3.05 |
| 18:30 | 2064 | Vjs vs HJS Akatemia | 2.26 | 3.78 | 2.55 |
| 18:30 | 2132 | EPS vs Salpa Salo | 3.29 | 3.44 | 1.98 |
| 18:30 | 2728 | Haka vs KuPS Kuopio | 3.49 | 3.49 | 1.90 |
| 19:00 | 2364 | Dodoma FC vs KMC | 1.29 | 4.53 | 9.65 |
| 19:00 | 4112 | Denmark W vs Norway W | 2.60 | 3.33 | 2.41 |
| 19:00 | 4590 | Torpedo Kutaisi vs Dila Gori | 2.94 | 3.48 | 2.12 |
| 19:00 | 5247 | FC Ilves-Kissat vs Grankulla Ifk | 1.89 | 4.22 | 2.99 |
| 20:00 | 1012 | Dinamo Batumi vs Dinamo Tbilisi | 2.15 | 3.30 | 3.20 |
| 20:00 | 2837 | CSKA Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.19 | 3.43 | 2.02 |
| 20:00 | 3411 | CRS Salmi vs Hassania Agadir | 2.95 | 2.85 | 2.44 |
| 20:00 | 3693 | Difaa El Jadidi vs Athletic Youssoufia | 2.50 | 2.99 | 2.74 |
| 20:00 | 3727 | Pyramids vs Enppi Club | 1.59 | 3.65 | 5.80 |
| 20:00 | 4085 | Ittihad Tanger vs MAS Maghrib A Fes | 2.81 | 2.71 | 2.66 |
| 20:00 | 4470 | FUS Rabat vs Rapide Oued Zem | 1.76 | 3.14 | 4.71 |
| 20:00 | 4952 | Raja Casablanca vs FAR Rabat | 1.89 | 3.20 | 3.88 |
| 20:00 | 5080 | Gomel vs Torpedo Zhodino | 2.20 | 3.25 | 2.95 |
| 20:00 | 5238 | Mouloudia Oujda vs Wydad Casablanca | 4.01 | 2.55 | 2.18 |
| 20:30 | 3751 | Saffle FF vs Lidkopings FK | 2.45 | 3.80 | 2.45 |
| 20:30 | 4335 | KI Klaksvik vs NSI Runavik | 1.04 | 9.82 | 26.52 |
| 21:00 | 1162 | Bragantino SP U20 vs Itapirense SP U20 | 1.73 | 4.10 | 3.90 |
| 21:00 | 2155 | Njarovik vs KF Fjallabyggd | 1.37 | 5.10 | 5.69 |
| 21:00 | 2987 | Huddinge IF vs IFK Eskilstuna | 1.50 | 4.61 | 4.61 |
| 21:00 | 3269 | Ponte Preta SP U20 vs CA Atletico Guacuano SP U20 | 1.14 | 7.20 | 15.00 |
| 21:00 | 3420 | Botafogo SP U20 vs Francana U20 | 1.27 | 5.40 | 9.00 |
| 21:00 | 3421 | CA Sao Jose Esporte SP U20 vs Flamengo SP U20 | 3.05 | 3.05 | 2.36 |
| 21:00 | 3448 | Corinthians SP U20 vs EC Sao Bernardo U20 | 1.27 | 5.11 | 8.65 |
| 21:00 | 3805 | CA Juventus SP U20 vs Nacional AC SP U20 | 1.83 | 3.60 | 3.95 |
| 22:30 | 1729 | Smouha Club vs Al Ahly Cairo | 5.63 | 4.12 | 1.53 |
| 22:30 | 4619 | RS Berkane vs Sccm Chabab Mohammedia | 2.01 | 2.94 | 3.82 |
| 22:30 | 5443 | Olympique Khouribga vs Olympique Safi | 2.23 | 2.85 | 3.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KICHUYA AZUNGUMZIA USAJILI WAKE SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Namungo Shiza Kichuya amesema mpaka sasa hakuna timu yoyote iliyomfuata kuhitaji saini yake, kwa hiyo bado ni mchezaji wa Namungo FC.

Mchezaji huyo pia ameeleza furaha yake kufunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi ya Jumapili iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, akisema kuwa hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kwake tangu aanze kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nimejisikia vizuri sana kufunga 'hat-trick' kwa sababu ilikuwa ni ya kwanza tangu nianze kucheza Ligi Kuu hapa Tanzania, halafu nimeifunga kwenye uwanja ambao ndiyo umenikuza na kunifanya nitambulike," alisema Kichuya, winga wa zamani wa Mtibwa Sugar na Simba.

**Kuhusu kupanda kwa kiwango chake, alisema kuwa yeye ni bora siku zote na siyo kama kiwango kilikuwa kimepungua.**

"Mimi ni bora siku zote hakuna siku utasema kiwango kimepanda au kushuka, ila Jumapili ilitokea, nikapata nafasi nikazitumia," alisema.

Alisema mpaka sasa hakuna timu yoyote ile ambayo imeshamfuata kutaka saini yake wakati huu ligi inapomalizika.

"Bado, hakuna timu yoyote iliyokuja kunihitaji, kwa hiyo mpaka sasa ni mchezaji wa Namungo," alisema Kichuya.

Kulikuwa na tetesi kuwa huenda mchezaji huyo akajiunga na Simba kwa ajili ya msimu ujao wa ligi, lakini hivi majuzi kukazuka tena tetesi kuwa Yanga na Azam FC zinapigana vikumbo kuwania saini yake.

Hata hivyo, klabu ya Yanga imeweka wazi kuwa haitosajili mchezaji yoyote wa ndani, badala yake inatarajia kusajili wachezaji wanne tu wa kigeni.



Msanii wa Muziki wa Kizazi Kipya, Maua Sama, akitumbuiza katikaTamasha la Kimataifa la Zege Day lililofanyika Temeke Mwembeyanga, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mabeyo azindua uwanja gofu wa kimataifa*

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Majeshi Tanzania, Jenerali Venance Mabeyo amesema uwanja wa gofu unaojengwa katika eneo la Ihumwa jijini Dodoma ni wa viwango vya Olimpiki, hivyo utasaidia kuvutia michezo ya kimataifa kufanyika hapa nchini hapo baadae.

Mabeyo alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Uwanja wa gofu ambao umebeba viwanja vya michezo mbalimbali ndani yake uliofanyika jana eneo la Ihumwa jijini Dodoma.

Mabeyo alisema uwanja huo ni wa kwanza kujengwa jijini hapa lakini ni wa pili wa mchezo wa Gofu kujengwa na jeshi hilo hapa nchini, ambapo wa kwanza ni ule uliopo Lugalo, Dar es Salaam.

Alisema lengo la kujenga viwanja vya michezo ni pamoja na kuisapoti serikali katika kuendeleza michezo hapa nchini, ili watanzania wazidi kuipenda michezo pamoja na kupanua wigo wa kushiriki mashindano ya kimataifa.

"Naomba niipongeze kamati ya Ujenzi wa uwanja huu iliyo chini ya Mwenyekiti Brigedia Hassan Mabena imefanya kazi nzuri ya ubunifu wa uwanja huo,"alisema Jenerali Mabeyo.

Naye Jenerali Mstaafu wa Jeshi hilo, George Waitara aliwataka Majenerali kujifunza kucheza gofu ili watumie uwanja huo badala ya kutumika na wageni pekee.

Alisema gofu ni mchezo wa kila mtu na kuitaka jamii kujitokeza kwa wingi kushiriki mchezo huo na kuachana na dhana ya kudhani mchezo huo unachezwa na matajiri pekee.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Gofu nchini (TGU), Chris Martine aliwashukuru Jeshi hilo kwa kusapoti michezo hapa nchini, husuani mchezo wa Gofu kwa kuendelea kujenga viwanja vya mchezo huo na michezo mingine.

# Michezo

Jumatano Juni 29, 2022

Nipashe




Chelsea wamfuata Sterling

UKURASA 21



Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo akipiga mpira wa gofu kama ishara ya uzinduzi wa uwanja unaojengwa eneo la Ihumwa, Dodoma. **PICHA NA RENATHA MSUNGU**

## Lewando ni suala la muda tu



**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier ...

HABARI UK. 22

## Origi atua rasmi AC Milan



**MILAN, Italia**

DIVOCK Origi amepigwa picha akiwa jijini Milan akijiandaa kukamilisha...

HABARI UK. 22

# Pazia Ligi Kuu kufungwa leo

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

● ● ● Timu tano zapambana kutoshuka daraja, msimu mpya...

LIGI kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 iliyoanza kutimua vumbi Septemba 27 mwaka jana inamalizika leo kwa timu zote 16 kukipiga kwa wakati mmoja, huku timu tano zikiwa kwenye hatari ya kushuka daraja au kucheza mechi za mchujo 'play off'.

**Ligi hiyo inatamatika leo huku bingwa tayari akiwa ameshapatikana ambaye ni Yanga ambayo mara ya mwisho kutwaa ubingwa ilikuwa ni msimu wa 2016/17, pia timu moja kati ya timu mbili zinazotakiwa kushuka daraja ikiwa imeshateremka.**

Timu hiyo ni Mbeya Kwanza ambayo si tu kwamba ni timu ya kwanza kushuka daraja msimu huu, lakini imeendeleza rekodi ya misimu kadhaa ya hivi karibuni Ligi Kuu kushusha angalau timu moja iliyokuwa imepanda msimu huo huo.

Ni Ligi iliyokuwa na ushindani mkubwa msimu huu, ingawa ni kwa timu 14 zilizobaki, lakini Yanga tangu mwanzo ilionekana kujiwekea ufalme wake, na baadaye Simba nayo ilionekana kujikatia kipande chake kwenye nafasi ya pili, hivyo kugawanyika katika makundi matatu.

Msimu huu ukiondoa Simba na Yanga, hakukuwa na timu iliyokuwa na uhakika wa kushinda mechi nyumbani, kwani kulikuwa na idadi ya mechi nyingi za timu kushinda ugenini tofauti na misimu kadhaa iliyopita.

Kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam, wenyeji Azam FC itacheza dhidi ya Biashara United, wakati kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, timu ya Dodoma Jiji itakipiga dhidi ya KMC, huku Ruvu Shooting ikiwa nyumbani, Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani itaikaribisha Prisons.

Kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, mwenyeji Kagera Sugar itamaliza msimu kwa kucheza dhidi ya Polisi Tanzania, huku Coastal Union ikipepetana na Geita Gold Uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga watakuwa nyumbani Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ikijaribu kuweka rekodi yake ya kumaliza ligi bila kupoteza mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, huku walionyang'anywa ubingwa Simba wakiwa ugenini, Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, kucheza na timu ambayo leo inaiaga rasmi ligi kwa kucheza mechi ya mwisho kabla ya kuhamia Championship, Mbeya Kwanza.

Kwa jinsi msimamo wa ligi ulivyo ni kwamba kuanzia timu iliyo kwenye nafasi ya 11, Dodoma Jiji yenye pointi 32, hadi ya 15 zipo kwenye hatari zaidi ya kushuka daraja au kucheza mechi za mchujo 'play off'.

Timu zingine zilizo kwenye hatari hiyo ni Mtibwa Sugar iliyo kwenye nafasi ya 12 kwa pointi 31, Ruvu Shooting ya 13, ikiwa pia na pointi 31, Prisons ya 14 ikiwa na pointi 29, na Biashara United nafasi ya 15 ikiwa na pointi 28.

Ni ushindi tu na kuombeana mabaya, ndiyo silaha itakayotumika kuziokoa timu mbili kati hizo kubaki salama, lakini moja itashuka daraja na mbili kwenda kucheza mechi za mchujo.

**NABI ANENA**

Kocha Mkuu wa Yanga, Nesredine Nabi amesema kutakuwa na mabadiliko makubwa kuelekea kwenye mchezo wao wa leo dhidi ya Mtibwa Sugar.

Kuelekea mchezo huo Yanga itawakosa wachezaji nane ikiwemo majeruhi pamoja na wengine kutumikia adhabu ya kadi tatu huku akisikitika kukosa kiungo wake, Zawadi Mauya ambaye ni majeruhi.

Mbali na majeruhi huyo lakini pia kuwepo kwa mechi ngumu ya fainali ya kombe la Shirikisho dhidi ya Coastal Union, itamlazimu kuwepo na mabadiliko katika kikosi cha timu hiyo.

Nabi alisema mechi dhidi ya Mtibwa Sugar ni ngumu kwa sababu wapinzani wao hao wanahitaji kuifunga Yanga kujinusuru kushuka daraja, lakini hao hawataki kupoteza rekodi yao kwa kupoteza katika mechi ya mwisho.

Alisema kuwepo kwa majeruhi na mechi ngumu ya fainali iliyopo mbele yao inamlazimu kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake kwa kuwapa mapumziko baadhi ya wachezaji wake waliotumika katika michezo mingi.

Alisema katika kuwasisitizia mechi ya Mtibwa Sugar ina umuhimu mkubwa kupata matokeo na ikitokea mchezaji akipuuza maneno yake atamchukulia hatua kali.

"Kuhusu Fiston Mayele hatuwezi kumpa presha katika mchezo wetu wa leo kwa sababu ya kufunga, endapo atafanikiwa kufunga na kuwa mfungaji bora tutafurahia lakini siwezi kumpa mzigo mkubwa wa kumlazimisha afunge kwa sababu tuna mechi ngumu ya fainali dhidi ya Coastal Union na tunategemea huduma yake katika mchezo huo," aliongeza Nabi.

Alisema kuhusu suala la ubora wa kikosi cha timu yake bado hawajafikisha asilimia 100 ya kiufundi kama alivyoahidi mwanzoni mwa msimu na sasa iko katika asilimia 70.

"Bado sijafikia asilimia 100 ya ubora wa kiufundi katika kikosi changu, nina imani siku zijazo unafikia asilimia 30 zilizosalia katika zile 70, walizofikia katika ubora wa kiufundi," alisema Nabi.

**KASONGO ATOA PONGEZI**

Kuelekea tamati ya msimu huu, Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania, Almas Kasongo amezipongeza klabu zote kufanikisha Ligi Kuu na Championship kumalizika salama.

Alisema msimu ujao itakuwa na mechi ya ufunguzi wa Ligi (kombe la Ngao ya Jamii), mchezo huo utakuwa Agosti 13, na ligi itaanza Agosti 17 mwaka huu.

"Tunatarajia kuanza msimu mpya wa 2022/23 kuanza rasmi Agosti 17 mwaka huu hadi Mei 27 mwakani tunatarajia kumaliza msimu, huku michezo ya Play off ikitarajiwa kuanza Juni 7 na 10, 2023," alisema Kasongo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >